# Uelekeo


*Leo yetu ndiyo kesho yetu*




**Presha ya kocha Robertinho yashuka**

Uk. 24

| ISSN 2953-2787 | Toleo Na. 00028 | Bei Tanzania sh 1,000 | Jumatano Septemba 6 - 12, 2023 |



KIMATAIFA
Uk. 19

## ECCAS yaipiga “stop” Gabon



SIASA
Uk. 12

## Katiba Mpya, tuhakikishe ni mhimili imara wa Watanzania



KOLAMU
Uk. 17

## Mambo matano ya kuzingatia kwenye maisha

# Mpango aanika mikakati ya kukabili uhaba wa chakula

Uk. 2

**Tunahitaji kukifanya kilimo kuwa cha kuvutia kwa vijana kwa kuweka miundombinu ya kisasa, kuwakopesha mitaji na kuwafungua katika masoko.**




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, jana akihutubia Wakuu wa Nchi mbalimbali, Wakuu wa Taasisi na Mashirika ya Kimataifa katika Mkutano wa Mabadiliko ya Tabianchi Barani Afrika (Africa Climate Summit 23) unaofanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Kenyatta (KICC), Nairobi nchini Kenya.

## Bashe aomba wawekezaji sekta ya kilimo

Uk. 2



## ‘Samia Rais mwenye maono makubwa’

Uk. 3

## Hospitali Muhimbili kupandikiza ini 2025

Uk. 3



# Mpango aanika mikakati ya kukabili uhaba wa chakula




**Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Philip Isdor Mpango akiwa ameshika Ripoti ya Hali ya Kilimo Afrika ya Mwaka 2018 (Africa Agriculture Status Report 2018) wakati akifungua rasmi Jukwaa la Mifumo ya Chakula 2023 jijini Dar es Salaam leo Septemba 5, 2023 katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julisu Nyerere (JNICC) jijini Dar es Salaam.**

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amesema Tanzania imejizatiti na kutekeleza hatua mbalimbali za kukabiliana na ukosefu wa chakula kwa kufanya mabadiliko ya mpango wa mfumo chakula ili kuongeza uwezo wa uzalishaji na kulifanya Taifa kuwa ghala la chakula ngazi ya kikanda na kimataifa.

Aliyasema hayo wakati akimwakilisha Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, katika ufunguzi wa Mkutano wa Mifumo ya Chakula barani Afrika (AGRF) jijini Dar es Salaam jana unaowashirikisha zaidi ya watu 3,000 kutoka nchi 70 duniani. Rais Dk. Samia anatarajiwa kufunga mkutano huo, Septemba 08, mwaka huu.

Alisema suala la mabadiliko ya mfumo wa chakula, limekuwa ajenda namba moja ya maendeleo nchini na Taifa limepiga hatua kubwa.

Huku akitoa mifano kadhaa, alisema sekta ya kilimo ni injini ya uchumi nchini ambapo inaajiri wastani wa asilimia 67 ya wananchi, kinachangia walau asilimia 30 ya fedha za kigeni kutokana na mauzo ya mazao nje ya nchi na kinachangia asilimia 65 ya malighafi ya viwandani.

Dk. Mpango alisema ili kufanisha mabadiliko ya uzalishaji wa chakula, serikali imeongeza bajeti ya kilimo kwa asilimia 70 kwa miaka miwili iliyopita kutoka Dola za Marekani milioni 120 kwa mwaka 2021/22 hadi Dola za Marekani milioni 397 kwa mwaka 2023/24.

Alisema ongezeko hilo la bajeti, limefanywa ili kubadilisha kilimo na kuwa cha kibiashara kuongeza bidhaa ya mazao hadi kufikia asilimia 10 ifikapo mwaka 2030 kutoka asilimia ya sasa ya 5.4.

Alisema mpango huo pia unalenga kuongeza huduma za ugani na uwekezaji katika sekta ya kilimo ili kuwashawishi vijana wengi kushiriki katika kilimo cha kibiashara kwa kuanzisha maeneo ya umwagiliaji chini ya programu ya Building a Better Tomorrow (BBT) inayolenga kuongeza ushiriki wa vijana katika kilimo kwa kuwapatia mafunzo, maeneo ya mashamba, mitaji na kuwaunganisha na fursa za masoko.

Alitaja mfano wa Chama cha Ushirika cha Wajasiriamali cha Wahitimu wa Chuo Kikuu cha Sokoine (SUGECO), kuwa ni moja ya mafanikio hayo ya kuwahamasisha vijana kushiriki katika sekta za kilimo, ufugaji na uvuvi.

Mapema, Makamu wa Rais Dk. Mpango alisema kila mtu ana haki ya kupata chakula, lakini kutokana changamoto kadhaa kama vile mabadiliko ya tabianchi, mlipuko wa ugonjwa wa Covid 19 na vita vinavyoendelea vya Urusi na Ukraine, haki ya upatikaji wa chakula kwa wengi imekuwa changamoto hususani kwa nchi nyingi za Afrika.

Inaendelea Uk. 4

## Bashe aomba wawekezaji kuwekeza sekta ya kilimo

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe, amewataka wawekezaji kuja kuwekeza nchini ili kumsaidia mkulima mdogo amudu kufanya kilimo chenye tija na kulifanya Bara la Afrika kujitegemea kwa chakula hata yanapotokea majanga duniani.




Akizungumza kwenye kikao kilichowakutanisha mawaziri wa kilimo na uvuvi kutoka Bara na Visiwani pamoja na wadau wa sekta kwenye kikao cha Mawaziri kuhusu Mkutano wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika (AGRF), kwenye ukumbi wa mikutano wa Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es Salaam jana alisema nchi imeweka mazingira mazuri kwa ajili ya uwekazaji.

"Mkulima ili aweze kuzalisha kwa tija, anahitaji mbegu bora, kuwa na uhakika wa mbolea kwa wakati na kwa gharama nafuu, lakini pia miundombinu ya maji ili aweze kuzalisha mara mbili mpaka tatu kwa mwaka," alisema.

Alisema changamoto kubwa ni mitaji, lakini pia uhakika wa mkulima kwenye kile anachokilima kwa wakulima wadogo hivyo wawekezaji wanapaswa kuweka mitaji yao ili kusaidia sekta hiyo kwani serikali imetenga ardhi ya kutosha kwa Kituo cha Uwekezaji (TIC) kwa ajili ya uwekezaji.

Inaendelea Uk. 4

# 'Rais Samia ni kiongozi mwenye maono makubwa'



**Na Claudia Kayombo, Singida**

MWANASIASA mkongwe mkoani hapa, Diana Chilolo, amesema Rais Samia Suluhu Hassan, ni kiongozi mwenye maono makubwa ya kiuongozi na kwamba hilo limedhihirika kupitia teuzi zake mbalimbali.

Diana amebainisha hilo baada ya hivi karibuni Rais Dk. Samia kufanya mabadiliko madogo ya Baraza lake la Mawaziri ambapo amesema wengi miongoni mwa aliowateua, anawafahamu kuwa ni wachapazi kwa kuwa alishawahi kufanya nao kazi.

Diana amesema baadhi ya watu wanaokosoa, watafurahishwa na matokeo chanya ya teuzi hizo.

Mwanasiasa huyo ambaye kitaaluma ni mwalimu na ameshawahi kushika nyadhifa mbalimbali ndani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Mbunge wa Viti Maalum katika awamu tatu kuanzia mwaka 2000 hadi 2015, aliyasema hayo mkoani hapa katika mahojiano maalum na UELEKEO.

"Katika uhalisia, Rais Samia anaonekana kuwa na mtazamo wa juu sana wa kiungozi, analenga hasa kuboresha uchumi na maendeleo ya Taifa letu, awali Watanzania wengi hawakutegemea hilo," alisema na kuongeza:

"Amekuwa mfano wa uongozi uliotukuka kwa Watanzania, amewajaza watu imani kuwa Rais mwanamke ni kama mama anayeweza yote, ameonesha uwezo wa kiuongozi wa kiwango cha juu."

Diana alisema anaamini hata katika chaguzi zijazo, CCM haitatumia nguvu kubwa kujinadi kwa kuwa kazi nyingi zimefanyika tena kwa ufasaha mkubwa, hivyo kuwarahisishia wagombea wa CCM kunadi sera zao.

Diana alikwenda mbali zaidi akisema kutokana na majukumu makubwa ya kiuongozi anayokabiliana nayo Rais Samia kwa Taifa, anamwombea kila uchao ili aendelee kudumu katika uongozi bora.

Alisema anamshukuru Mungu kwa kuwezesha Rais Samia kupata madaraka hayo makubwa, nafasi ambayo haikuwahi kushikwa na wanawake kutokana na mfumo dume uliokuwa ukilitafuna Taifa na dunia nzima kwa muda mrefu.

Alisema hilo lilitokana na wengi kutoamini iwapo kinamama wanaweza kuwa mfano wa uongozi bora na kwamba Rais Samia ameondoa fikra hiyo.

Aliongeza kuwa Rais Samia ameonesha uchapa kazi wake mahiri na hivyo kuifanya jamii izidi kuusukumia pembezoni mfumo dume uliokuwa ukiwaweka kando wanawake wengi kwa muda mrefu ambapo hawakuwa wakiaminiwa kupewa madaraka makubwa kama hayo.

Akijibu iwapo amejipanga kugombea nafasi ya uongozi katika uchaguzi wa mwakani na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025, alisema hafikiri labda akishawishiwa.

Hata hivyo, Diana alisema yupo tayari kufanya kazi yoyote iwapo Rais atamteua kwani ataifanya kwa ufasaha mkubwa, kwa kuwa asili yake anapenda kusifiwa kutokana na kutekeleza majukumu yake kwa ufasaha.

"Mheshimiwa Rais wetu, akiona nafaa kufanya majukumu yoyote ya kiserikali, naahidi nitayafanya tena vizuri sana," alisema na kuongeza:

"Rais akiniteua, nitachapa kazi, nitafanya kazi kwa mfano na uadilifu. Kwani mimi huwa napenda kusifiwa, na kwa kuwa nguvu na nia ya kufanya kazi ninayo, nitafanya kwa ufasaha mkubwa. Hata nafasi nilizowahi kushika, nimeacha historia nzuri, nilizitendea haki ilivyostahili," alisema.

# Hospitali Muhimbili kupandikiza ini kufikia mwaka 2025



**Na Mwandishi Wetu**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH), itaanzisha huduma ya upandikizaji ini ifikapo mwaka 2025.

Hatua hii ni mwendelezo wa azma ya serikali kuhakikisha kwamba huduma za ubingwa bobezi, zinapatikana nchini.

Hayo yalielezwa na Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Profesa Mohamed Janabi, wakati akifungua mafunzo ya awali ya uchunguzi na matibabu ya magonjwa ya ini yaliyofanyika hospitalini hapo kuelekea kwenye kongamano la wataalamu wa magonjwa ya ini Barani Afrika (COLDA) linalotarajiwa kufanyika kesho hadi Septemba 9, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Profesa Janabi alisema katika kuelekea hatua ya upandikizaji ini, mafunzo mbalimbali ya wataalamu yanaendelea kutolewa kupitia kituo cha kutoa mafunzo, uchunguzi na matibabu ya kibobezi ya Magonjwa ya Mfumo wa Chakula na Ini katika Ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara Afrika kilichopo MNH.

Kituo hicho kilianzishwa mwaka 2012 kwa ushirikiano na ufadhili wa Taasisi ya Munich Foundation ya Ujerumani, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili na hivyo kuifanya hospitali kuwa miongoni mwa vituo vichache vyenye hadhi ya namna hiyo Barani Afrika.

Vituo vingine vipo Rabat, Morocco, Johannesburg, Afrika ya Kusini na Cairo nchini Misri.

Alisema kuwa kongamano la wataalamu wa magonjwa ya ini Barani Afrika, ni moja ya maandalizi ya kusaidia huduma za upandikizaji ini kuanza kufanyika nchini kwa kuwa litatoa fursa ya wataalamu kujifunza, kujadili na kupanga mwendelezo wa mafunzo ya mara kwa mara ya ndani na nje ya nchi ambayo yatawajengea uwezo kuanzisha huduma ya upandikizaji ini nchini.

"Hii safari ni ndefu na nzito, lakini tunaamini kwa msaada wa serikali na wadau mbalimbali, tutafanikiwa kwani hadi sasa kituo kina uwezo wa kutoa huduma kwa wagonjwa waliofanyiwa huduma hiyo nje ya nchi wanaporejea hapa nyumbani tofauti na awali ambapo walilazimika kurudi nje ya nchi. Jambo hili linakwenda sambamba na uboreshaji wa maabara za kiuchunguzi wa patholojia, uchunguzi wa damu, uchunguzi wa radiolojia na tiba radiolojia na uboreshaji wa vyumba vya wagonjwa mahututi," alisisitiza Profesa Janabi.

# Mpango aanika mikakati ya kukabili uhaba wa chakula



Inatoka Uk. 2

Alisema kwa mujibu wa ripoti ya Usalama wa Chakula na Lishe ya Julai, mwaka huu, mtu mmoja kati ya watu watano Afrika, anakabiliwa na njaa, hii ikiwa ni zaidi ya mara mbili ya wastani wa idadi ya watu duniani.

Kuhusu Afrika, Dk. Mpango alizitaka nchi hizo kuvuna ujuzi wa kisayansi ikiwemo teknolojia asili za kuzalisha na kuchakata chakula cha kutosha kwa watu wake na pia kwa mahitaji ya soko la kimataifa.

Aidha, alisema mataifa ya Afrika yanahitaji kuchukua njia muafaka kuwawezesha wakulima wadogo wadogo kwa kuwapa pembejeo kwa gharama nafuu, elimu na ujuzi na kuwawezesha kupata fedha ili kuongeza tija.

Pia alisema nchi hizo zinatakiwa kufanya utafiti wa kisayansi kwa kuzingatia hali ya sasa ya mabadiliko ya kidigitali.

Alizitaka nchi hizo kuwawezesha vijana na wanawake ambao idadi yao inaongezeka na kuwa kama chachu na uti wa mgongo wa uzalishaji wa chakula katika nchi zao.

"Tunahitaji kukifanya kilimo kuwa cha kuvutia kwa vijana kwa kuweka miundombinu ya kisasa, kuwakopesha mitaji na kuwafungua katika masoko. Pia kilimo cha mbogamboga na matunda, ni kizuri kwa sababu kinalipa kwa haraka," alisema.

Aidha, alizitaka nchi hizo kukomesha vitendo vya unyonyaji kwa wakulima kwa kutumia vipimo na mizani vilivyothibitishwa kununulia mazao ili kuwalinda.

Alisema kwa mfano, Tanzania imefanikiwa kudhibiti unyonyaji huo katika mnyororo wa thamani kwa mauzo ya nyama, mchele na maharage na nguvu zinaendelea kudhibiti katika mazao mengine.

Alisema sekta ya kilimo na ufungaji, inahitaji mazingira ya amani na utulivu ambayo ni muhimu kwa uzalishaji na kupata tija.

Mkutano huo umekutanisha watu wa kada mbalimbali kama viongozi wa nchi, watu maarufu, vijana, watalaam wa kilimo, watunga sera, wafanyabiashara, wawekezaji, wakulima, wafugaji na wavuvi kutoka kila sehemu mbalimbali duniani.

# Ujenzi wa daraja wazima kilio cha wananchi Ifucha

**Na Allan Vicent, Tabora**

KUKAMILIKA kwa ujenzi wa mradi wa Daraja la Upinde wa Mawe katika Kijiji cha Ifucha, Kata ya Ifucha Halmashauri ya Manispaa Tabora, kumesaidia kumaliza kilio cha muda mrefu cha wakazi wa kata hiyo kupoteza mali zao katika eneo hilo kwa kusombwa na maji.

Akizungumza na gazeti hili jana, Naibu Mstahiki Meya wa Halmashauri ya manispaa hiyo ambaye ndiye Diwani wa kata hiyo, Rose Kilimba, alisema daraja hilo mbali na kuwa kivutio kizuri kwa wapitaji, pia limeleta neema kwa wananchi.

Alisema kabla ya kujengwa daraja hilo eneo hilo lilikuwa hatarishi kwa wakazi wa kata hiyo na kata jirani ya Itonjanda kwa kushindwa kupita hasa wakati wa masika kutokana na maji kufurika na hivyo kusababisha usumbufu mkubwa kwa wanachi.

Aliongeza kuwa wakazi wengi wa kata hizo walipoteza mali zao na baadhi yao kupoteza maisha kwa kusombwa na maji, hali iliyosababisha eneo hilo kuwa hatarishi na kikwazo kikubwa kwa maendeleo.

"Tunamshukuru sana mama yetu, Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kusikia kilio cha wananchi na kuwapatia Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (Tarura) kiasi cha Sh. milioni 149.4 ili kujengwa daraja hilo, kilio cha wananchi sasa kimeisha," alisema.

Naibu Mstahiki Meya alifafanua kuwa kukamilika kwa daraja hilo, kumerahisisha kwa kiasi kikubwa huduma za usafiri na usafirishaji bidhaa na mazao ya kilimo katika vipindi vyote vya majira ya mwaka kwa wakazi wa kata hizo.

Akielezea mradi huo, Meneja wa Tarura Wilaya ya Tabora Mjini, Mhandisi Manyama Tungaraza, alisema aina hiyo ya ujenzi wa madaraja ni nafuu sana ikilinganishwa na madaraja yanayojengwa kwa nondo na zege.

**Tunamshukuru sana mama yetu, Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kusikia kilio cha wananchi na kuwapatia Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (Tarura) kiasi cha Sh. milioni 149.4 ili kujengwa daraja hilo, kilio cha wananchi sasa kimeisha.**

Alibainisha kuwa ujenzi wa daraja la upinde wa mawe hutumia makunzi ya mawe na saruji pekee pasipo kuweka nondo na zege, na kubainisha kuwa kama wangetumia nondo na zege, lingegharimu zaidi ya Sh. milioni 375.

Aliongeza kuwa daraja hilo ni imara zaidi na litatumika kwa miaka mingi bila kuharibika na kutoa wito kwa wakazi wa kata hizo kutopitisha mifugo yao kwenye barabara zinazojengwa katika maeneo yao ikiwemo daraja hilo.

Mhandisi Manyama alieleza kuwa mradi huo umekamilika kwa asilimia 100 na umeanza kutumika pamoja na ujenzi wa vipande viwili vya barabara zinazounganisha daraja hilo pande zote mbili.

# Bashe aomba

Inatoka Uk. 2

"Tumekutana hapa Mawaziri wa Kilimo ili kuwaonesha wawekezaji mahali pa kuwekeza, kuboresha sekta hii kwani sasa hivi kilimo kimeshakua biashara na ndiyo maana tumefungua milango kwa mkulima kuuza mazao yake popote," alisema.

Aliongeza kuwa, kupitia mkutano huo wa AGRF, wataionesha dunia fursa zilizopo nchini katika sekta ya kilimo ili kuhakikisha nchi inalima kwa, lakini pia inaacha utegemezi wa chakula na badala yake inauza kwenye mataifa mengine.

Kwa upande wake, Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema kujikita kwenye sekta ya kilimo kutasaidia kupunguza ukosefu wa ajira kwa vijana, lakini pia kupunguza kutumika fedha nyingi kuagiza chakula kutoka nje.

Alisema kilimo sasa kimekuwa sekta ya biashara, hivyo kinapaswa kutumiwa ili kubadilisha maisha ya vijana kwani nchi inakwenda kujitegemea katika chakula, lakini pia kuzalisha ajira nyingi hali itakayosaidia kuzalisha walipa kodi wengi.

"Idadi ya watu wanaohitaji ajira, ni kubwa hivyo juhudi za serikali ni kuingiza vijana wengi na wanawake kwenye sekta ya kilimo kwani sasa hivi kilimo kimekuwa biashara hivyo mapato ya serikali yataongezeka ikiwa sekta hii itakua na kuwekezwa ili izalishe kisasa," alisema Dk. Mwigulu

Naye Waziri wa Uvuvi na Mifungo, Abdallah Ulega, alisema ili kuboresha sekta ya kilimo, uvuvi na mifugo teknolojia, masoko na mitaji inahitajika, hivyo wawekezaji wanapaswa kuwekeza ili kukuza sekta hiyo kuzalisha kwa tija na kuuza nje.

Mkutano wa Mifumo ya Chakula Afrika AGRF unafanyika jijini Dar es Salaam ambapo unahudhuriwa na watu zaidi ya 3,000 kutoka mataifa mbalimbali Afrika.

# Mlalakuwa wapambana katika usafi

**Na Selina Mpapa,TUDARCo**

SERIKALI ya Mtaa wa Mlalakuwa, Kata ya Kawe, jijini Dar es Salaam, imeanza kutekeleza kazi ya ukusanyaji takataka ili kuweka mtaa huo kuwa na mazingira bora zaidi na kuzuia magonjwa ya mlipuko.

Mwenyekiti wa mtaa huo, Suleimani Masare, alisema anatoa rai kwa kuwaomba wananchi kukusanya takakata na kuzuia zisizagae kwenye barabara za mitaa.

Aidha, aliwataka waitikie wito wa kuchangia gharama za uzoaji takataka katika mtaa huo na kwamba hawatakiwi kuwa wagumu kushiriki masuala ya kijamii inayowazunguka.



**Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, akizungumza katika kikao cha Mawaziri kuhusu Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika (AGRF) kabla ya Wakuu wa Nchi za Afrika jijini Dar es Salaam jana.**




**Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, akizungumza katika kikao cha mawaziri hao jijini Dar es Salaam jana.**



**Mawaziri na viongozi mbalimbali, wakishiriki na kufuatilia hotuba mbalimbali zinazoendelea katika mkutano huo.**

# Maoni ya Mhariri & Uchambuzi

## HII NI KERO

### Uvaaji mavazi yasiyo na maadili



KUNA baadhi ya watu hususan vijana wana tabia ya kuvaa mavazi yasiyo na maadili katika jamii. Utakuta binti wa kike anavaa nguo fupi na zinazobana, huku vijana wa kiume wakivaa nguo chini ya makalio kuonesha nguo za ndani.

Hayo si maadili yetu sisi Watanzania wenye kujali mila na desturi zetu.

Ushauri wangu kwenu ni muhimu kuvaa nguo zenye staha ili kulinda heshima na thamani ya utu wako kwani utakuwa kielelezo kizuri kwa jamii inayokuzunguka.




MAONI YA MHARIRI

# Tuchangamkie fursa tele za Mkutano wa AGRF

MKUTANO wa Mifumo ya Chakula Afrika (AGRF), ulifunguliwa rasmi na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Philip Mpango, jijini Dar es Salaam jana.

Mkutano huu unajadili suluhu za uhakika na usalama wa chakula Barani Afrika.

Tanzania ni mwenyeji wa mkutano huu kutokana na hatua kubwa za kimageuzi ambazo Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, imezichukua tangu alipoingia madarakani miaka miwili iliyopita.

Hatua hizo ni pamoja na kuongeza bajeti ya Wizara ya Kilimo mara nne kwa mwaka wa fedha 2022/2023, kuwekeza katika miundombinu ya umwagiliaji, huduma za ugani, pembejeo na ruzuku ya mbolea na mbegu kwa viwango vya juu ili kuimarisha sekta ya kilimo kwa maendeleo ya nchi.

Mkutano hu umewakutanisha watu zaidi ya 3,000 wakiwemo viongozi, watunga sera, wanasayansi, wakuu wa serikali na taasisi za binafsi, wakulima na vijana.

Kupitia mkutano huu, Tanzania itapata fursa ya kuonyesha mafanikio yake katika sekta ya kilimo na chakula, kujifunza kutoka kwa wadau wengine wa sekta hiyo na kuweka mikakati endelevu ya kuimarisha usalama wa chakula barani Afrika.

Ushiriki mkubwa wa viongozi wakuu wa nchi, mawaziri wa kilimo na wanasayansi waliobobea katika masuala ya kilimo, utatoa fursa kubwa kwa Tanzania kujifunza mengi yahusuyo masuala ya mifumo ya kilimo na usalama wa chakula nchini.

Kwa msingi huo, hii ni fursa adhimu na muhimu mno kwa Watanzania kuhakikisha fursa hii wanaitumia vyema katika kuvuna mbinu mbalimbali za kilimo hasa kwa kuzingatia kwamba wataalamu wa kutoka mataifa kadhaa duniani yalibobea katika kilimo cha mazao ya kila aina, wanatoa mada kwenye mkutano huu.

Ni wajibu wa kila mkulima na Mtanzania, kufungua masikio yake kufuatilia na kusoma mada hizo ili hatimaye zitumike kwa vitendo katika kujiongezea tija katika kilimo cha mazao ya chakula pamoja na ya biashara.

UELEKEO kama ilivyo wajibu wetu, tutazianisha mada hizo kwa lugha rahisi na ya kueleweka, ili kuwasaidia wakulima wa Tanzania wanufaike na mkutano huu muhimu Barani Afrika.

## Wasiliana nasi

**Mhariri Mkuu:** +255713263775 / +255748115000
**Mhariri wa Habari:** +255753333330
**Mhariri Michezo:** +255787559090
**Meneja Masoko/Biashara:** + 255718480406 / + 255733768825
**S. L. P:** 15110, Dar es Salaam
**Makao Makuu Mtaa:** Barabara ya Morogoro
**Jengo la:** Aura Mall
**Chumba Cha Habari:** +255 (0)222151532
**Email:** uelekeohabari@gmail.com



Na Godfrey Sanga
Sangagodfrey26@gmail.com

JICHO LANGU

# Dini zetu ni umoja wetu

MOJA ya sababu kubwa kwa Watanzania kutoyumbishwa, kubabaishwa na kutengana, ni uwepo wa dini nyingi unaohimiza amani, upendo, uzalendo na kuwajibika.

Kwa lugha nyepesi ninaweza kuitafsiri dini kama jumla ya imani ya binadamu kadhaa pamoja na mafundisho wanayotoa kuhusu yale ambayo wanayazingatia ama kuyasadiki (kuamini), yaani mambo ya roho, kuhusiana na Mungu, maisha na uumbaji.

Ibada inatajwa kuwa nguzo mojawapo iliyo dhahiri miongoni mwa dini kadhaa katika kuunganisha dhamira za anayeshika dini na mhimili wa imani, lakini dini inahusu pia mafundisho kuhusu maadili, mema na mabaya, imani na jinsi ya kushiriki katika jumuiya za waumini.

Tangu nyakati za zamani, binadamu tumejaribu kuangalia kote na kuchunguza juu yetu na kujiuliza kuhusu anga, ulimwengu na maana ya maisha.

Tofauti na wanyama, wanadamu waliumbiwa haja ya ndani ya kutaka kuelewa jinsi tulivyofika hapa duniani, kwa nini tuko hapa na nini kinachotokea baada ya kufa.

Pamoja na hayo kila mmoja wetu kwa imani yake hutambua namna gani na jinsi ambavyo dini yake ilivyoanza na kuingia hapa nchini.

Wengi wetu ni mashuhuda, kuna nchi nyingi zimekosa amani, utulivu na kukumbwa na maafa yanatokea kwa sababu ya kila mtu kuona dini yake ndiyo bora na kudharau watu wa dini nyingine (udini).

Wakati wa uhai wake, Mwalimu Julius Nyerere alikemea hali ya udini.

> **Tangu nyakati za zamani, binadamu tumejaribu kuangalia kote na kuchunguza juu yetu na kujiuliza kuhusu anga, ulimwengu na maana ya maisha. Tofauti na wanyama, wanadamu waliumbiwa haja ya ndani ya kutaka kuelewa jinsi tulivyofika hapa duniani, kwa nini tuko hapa na nini kinachotokea baada ya kufa.**

Akihutubia mkutano wa mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wa kumtafuta mgombea urais kupitia chama hicho 1995, na Machi 13 mwaka huo huo, Nyerere alisisitiza kutoingiza udini katika uongozi wanchi.

"Tunataka Rais wetu akiwa Mkristo, ajue hatumchagui kwa sababu ya Ukristo wake, na kama Mwislamu hatumchagui kwa sababu ya Uislamu wake na tunataka hilo alijue na alikubali kwa dhati na alisaidie," alisema.

Jicho langu limefunguka na kuona kwamba, Tanzania tunasifika kuwa nchi ya amani na upendo kwa sababu ya misingi imara ya kutobaguana kwetu tangu zamani hali iliyopelekea wote kujiona kuwa jamaa moja wenye lengo la kuijenga Tanzania moja bila kujali misingi ya udini na ukabila.

Pongezi kwa viongozi wote wa dini bila kujali misimamo na madhehebu yao, kwakuendelea kuiendeleza kauli ya Hayati nyerere kwa vitendo kila uchwao.

Ni muhimu kutambua kwamba njia pekee ya kuitunza tunu ya amani yetu ni kuweka udini kando na kuwakataa wale wote wenye nia au dhana ya kuondosha umoja wetu kwa kuleta udini.

Jicho langu linakukumbusha wewe muumini wa dini au dhehebu fulani kuwa njia pekee ya kuondokakana na mifarakano, adha na usumbufu ni kutobaguana kwa sababu ya dini zetu.

Kazi Iendelee.

# Waziri Ummy awapa neno watendaji sekta ya afya

**Na Mwandishi Wetu, Dodoma**

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amewataka watendaji ndani ya sekta ya afya, kufanya kazi kwa ushirikiano ili kuleta tija katika kuboresha ubora wa huduma za afya nchini.

Waziri Ummy aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na Menejimenti ya Utumishi ya Wizara ya Afya kuhusu mipango ya utekelezaji wa hatua za kufikia vipaumbele 14 vilivyowekwa na wizara hiyo kwenye bajeti ya mwaka 2023/24.

"Dhamira yangu ni kuboresha ubora wa huduma za afya nchini, tufanye kazi kwa ushirikiano na kuweka mbele maslahi ya sekta ya afya na Tanzania," alisema Waziri Ummy.

Ummy alisisitiza watendaji ndani ya sekta ya afya wanatakiwa kuijua vyema sekta hiyo na kufanya mambo yenye tija katika kuboresha huduma za afya kwa wananchi.

Alisema Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, amefanya kazi kubwa kuboresha sekta ya afya kwenye miundombinu ya kutolea huduma za afya, ununuzi wa dawa, vifaa na vifaa tiba, ajira za watumishi pamoja na kusomesha wataalam, hivyo, ni wajibu wa watendaji ndani ya sekta hiyo kuhakikisha wanaboresha huduma za afya wanazotoa kwa wananchi.

"Sekta ya afya ina fedha nyingi na wadau wengi wanaofanya kazi, naomba tuelekeze fedha hizo katika kuboresha huduma za afya ili wananchi wanufaike na upatikanaji wa huduma bora za afya," alisisitiza Waziri Ummy.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Dk. John Jingu, alisisitiza watendaji ndani ya Wizara na sekta ya afya kwa jumla, wanatakiwa kufanya kazi kwa umoja na kushirikiana katika kutoa huduma bora kwa wananchi.

Dk. Jingu alisema watendaji wana dhamana kubwa ya kutatua kero za wananchi, hivyo wanatakiwa kuwa na ushirikiano wa karibu katika kuhudumia wananchi ili kuleta tija katika uboreshaji wa huduma za afya nchini.



# Veta yatamba ilivyoiinua Singida kwa ufugaji

**Na Claudia Kayombo, Singida**

CHUO cha Ufundi Stadi (Veta) mkoani Singida, kimesema kimewezesha sekta ya ufugaji kupiga hatua kubwa mkoani hapa hasa baada ya kuanzisha kitengo cha ufugaji mwaka 2012.

Mkuu wa kitengo hicho, Hamisi Msangi, amesema awali wafugaji wengi wa kuku wa kienyeji mkoani hapa, hawakufuga kwa tija kwani waliwaacha wajiokotee wenyewe vyakula au kuwapa chakula cha aina moja.

Msangi alibainisha hilo wiki iliyopita katika mahojiano maalum na gazeti hili chuoni hapo.

"Kwa sababu Singida inasifika kwa ufugaji wa kuku wa kienyeji, tulianza kwa kuwauzia wafugaji vyakula kwa bei nafuu huku tukiwapa elimu ya umuhimu wa vyakula hivyo kwa mifugo yao.

"Tuliona tuwape elimu baada ya kubaini kuwa wengi hawakuwa na utaratibu wa kuwapa lishe bora wanyama hao, walikwapa cha aina moja.

"Vyakula vyetu vilikuwa na virutubisho vinavyohitajika kwa ukuaji wa kuku na mazao bora, hivyo tuliwashawishi wafugaji waje wapate kozi za muda mfupi kuwawezesha kuendesha ufugaji wenye tija. Mwitikio ulikuwa mkubwa.

"Kwa sababu wengi walikuwa wanafuga kwa mazoea, tulipokuja na hii program, sasa wananunua vyakula vyenye virutubisho kwa ajili ya kuku wao, wengine hutengeneza wenyewe baada ya kupata elimu hapa," alisema na kuongeza: "Maeneo mengi sasa wafugaji wanafanya ufugaji wa kibiashara, wanatengeneza vyakula bora kwa ajili ya kuku au wananunua kutoka katika kampuni mbalimbali zinazozalisha vyakula vya Mifugo."

Anabainisha kuwa ni dhahiri elimu hiyo imechochea mapinduzi katika sekta ya ufugaji hususan wa kuku kwani wengi wanafuga kwa tija na hivyo kupata pato linaloboresha maisha ya familia zao.

Alisema mwanafunzi hujifunza pamoja na mambo mengine, vyakula vinavyofaa kwa ajili ya mnyama husika, lakini pia namna ya kumtibu anapobainika kuathiriwa na magonjwa.

Aidha, Msangi alisema chuo hicho hakitoi mafunzo ya ufugaji kuku pekee bali ng'ombe, mbuzi, kondoo, nguruwe, sungura, bata wa nyumbani na bata mzinga.

Pia chuo kipo katika mchakato wa kuanzisha ufugaji wa kwale, kuendeleza ufugaji wa kanga, bata bukini pamoja na ndege wengine ambao hawapo kwa sasa chuoni hapo lengo ni kuwawezesha wanachuo kufahamu tabia zao na namna ya kuwafuga ili baada ya kuhitimu, wakaendeleze maarifa hayo wakiwa na uhakika wa kile wanachokifanya.

Mwanafunzi Ridhael Munuo, wa mwaka wa kwanza katika fani hiyo, alisema anajisikia fahari kubwa kuchukua maarifa yanayohusu ufugaji ,kwani licha ya kuwa yupo mwaka wa kwanza, lakini amebaini kuwa mafunzo kuhusu wanyama ni mazuri mno.

Alisema ana amini iwapo vijana wengi watajikita kutafuta maarifa kuhusu utunzaji wa wanyama, suala la ajira kwao halitakuwa tatizo.

Mfugaji Isack Evod, mkazi wa Mwenge mjini hapa, aliishukuru Veta Singida kwa kubadilisha maisha yake.

"Binafsi mimi najivunia elimu niliyopata katika Chuo cha Veta Singida, nawashauri wafaugaji wenzangu waende kupata elimu ya ufugaji kwani ufugaji bila elimu ni hasara," alisema Evod.

"Sasa nina kuku machotara zaidi ya 273 ambao natarajia kuwauza hivi karibuni, kila mmoja ninamuuza kwa bei ya Sh. 15,000, sikosi fedha za matumizi," alisema Evod.

Kaimu mkuu wa Chuo hicho, Alphoncina James, alitoa wito hususan kwa wakazi wa Singida, kujitokeza kwa wingi kusoma kozi mbalimbali za muda mfupi na mrefu zinazotolewa na chuo hicho. Alphoncina alisema Veta imejipanga kupokea idadi ya wanachuo wengi ili kuwapa maarifa



# Ashinda rufaa dhidi ya kesi ya ubakaji

**Na Selina Mpapa, TUDARCo**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam, imemuachia huru Miraji Omari, aliyedaiwa kumbaka msichana mwenye umri wa miaka 15 na kuhukumiwa kifungo cha miaka 30 katika Mahakama ya Wilaya Temeke, baada ya rufaa yake kupinga kifungo hicho kukubaliwa.

Mahakama hiyo imemfutia hatia na adhabu mshitakiwa huyo aliyedaiwa kutenda kosa hilo Agosti 7, mwaka 2020 akiwa katika nyumba ambayo haijakamilika kujengwa.

Hakimu Mkazi Mkuu, Amiri Msumi, alisema: "Anakubalina na rufaa ya mshtakiwa huyo kwa sababu upande wa mashitaka ulishindwa kuthibitisha mashitaka dhidi ya mshtakiwa na ushahidi haukujitosheleza."

Aidha, Hakimu Msumi alisema, ushahidi ulitolewa na muathirika, una mapungufu kadhaa na hauoneshi kwa undani ni namna gani alikuwa akibakwa.


Alisema katika utetezi wake muathirika alidai kuwa alibakwa katika nyumba ambayo hajaisha, lakini shahidi namba tano ambaye ni mpelelezi , alidai alipokwenda kutembelea nyumba hiyo, alikuta imekamilika hivyo kuna ukinzani katika ushahidi huo.

Pia alisema muathirika ambaye ni shahidi namba moja, hakueleza nyumba hiyo iko maeneo gani, na kama kulikuwa na majirani gani, na iko umbali kiasi gani kutoka saluni alipokuwa akitoka mshtakiwa hadi katika nyumba hiyo.

Vilevile, alisema shahidi huyo hakuwa na maelezo mengine mbali na kusema amebakwa na mtu huyo na hakuna uhusiano wowote unaothibisha kwamba alibakwa zaidi ya maneno ya mdomoni.

"Nathubutu kusema upande wa mashitaka, haujathibitisha na ushahidi umeshindwa kuthibitisha mashitaka hayo," alisema Hakimu Msumi.

Aliongeza kuwa anakubaliana na rufaa hiyo na anamuondolea mshtakiwa huyo adhabu ya kifungo cha miaka 30 jela, pia ameamuru aondolewe jela isipokuwa kama ana kosa lingine.




# Meno ya tembo yamtupa jela miaka 20

**Mahakama imepitia utetezi wa washtakiwa wote wawili na umetupilia mbali shitaka la mshtakiwa namba mbili kwa kuwa upande wa mashitaka, umeshindwa kuleta ushahidi uliokamilika dhidi yake, hivyo, mahakama inamuachia huru James Jeremiah,**



**Na Shamila Mkomweke, TURDACo**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam imemhukumu Jumanne Hamisi, kifungo cha miaka 20 jela na faini ya zaidi Sh. bilioni moja baada ya kupatikana na hatia ya kukutwa na meno manane ya tembo ambayo ni nyara za serikali.

Hata hivyo, mahakama hiyo imemuachia huru James Jeremiah.

Hukumu hiyo ilitolewa na Hakimu Mkazi Mkuu Yuston Ruboroga, wa mahakama hiyo.

James na Jumanne, kwa pamoja walikuwa wakikabiliwa na kosa la kukamatwa na nyara za serikali vikiwemo vipande vinane vya meno ya tembo.

"Mahakama imepitia utetezi wa washtakiwa wote wawili na umetupilia mbali shitaka la mshtakiwa namba mbili kwa kuwa upande wa mashitaka, umeshindwa kuleta ushahidi uliokamilika dhidi yake, hivyo, mahakama inamuachia huru James Jeremiah," alisema Hakimu Ruboroga.

Hakimu Ruboronga alisema Jumanne anaruhusiwa kukata rufaa kama hajaridhika na maamuzi ya Mahakama.

Jumanne alitiwa mbaroni baada ya kukamatwa na vipande vinane vya meno ya tembo Machi 3, mwaka 2017 wilayani Temeke jijini Dar es Salaam.

# Atupwa miaka 30 jela kwa kusafirisha bangi

**Na Mwandishi Wetu**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Morogoro, imemhukumu Awadhi Mohamed, kifungo cha miaka 30 jela baada ya kukutwa na kosa la kusafirisha kilo 34.65 za dawa za kulevya aina ya bangi na imeamuru bangi hiyo iteketezwe.

Hukumu hiyo ilitolewa wiki iliyopita na Hakimu Mkuu Mkazi, Livini Benedict.

Hakimu Benedict alisema mahakama yake imetoa adhabu hiyo kwa mujibu wa sheria na pia liwe fundisho kwa wote wanaojihusisha na biashara ya dawa za kulevya.

Mapema, ilidaiwa kuwa Desemba 22, mwaka 2022, mshtakiwa alikamatwa na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya katika Kijiji cha Chogoali Sokoni, Kata ya Iyongwe, Wilaya ya Gairo mkoani Morogoro akiwa na kilo 34.64 za bangi iliyohifadhiwa katika mifuko ya plastiki maarufu kama sandarusi.



Jarida hili haliuzwi

*Leo ndiyo, kesho yetu*

Uelekeo

JARIDA

# Jungu kuu

| Jumatano Septemba 6 - 12, 2023 |




# Katiba Mpya, tuhakikishe ni mhimili imara wa nyumba ya Watanzania

UK. 12 & 13



UK. 14

UK. 16

## Uchumi



# Chunya ilivyojikita kuongeza uzalishaji dhahabu

**Na Hellen Mwango, aliyekuwa Chunya**

UZALISHAJI mkubwa wa madini ya dhahabu Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, umesababisha Tume ya Madini kuipatia wilaya hiyo hadhi ya Mkoa wa Kimadini na hivyo kuitwa Mkoa wa Kimadini Chunya.

Hatua hiyo inaipa nguvu Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kupitia watendaji wake kuandaa utaratibu maalum kwa ajili ya kusambaza umeme kwa wachimbaji wa madini ya dhahabu wa kati na wadogo wilayani.

Masuala hayo yakiwa sawia, kutakuwa na kasi ya ongezeko la ajira, hususani za kujiajiri. Wachimbaji watajikomboa kiuchumi wao pamoja na familia zao na pia kuongeza pato la taifa kupitia ulipaji kodi.

Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Kimadini Chunya, Sabai Nyansiri, anaeleza kwa waandishi wa habari wa Uhuru Media Group katika migodi ya wachimbaji wa kati wilayani humo kuwa wamefanya kazi kubwa kuwajengea uwezo wachimbaji hao na pia imewapa mwongozo wa uchimbaji.

Anasema Chunya ina wafanyabiashara wengi, wachimbaji wakubwa wenye leseni wapo 70 na wachimbaji wadogo wapo 300 na kwamba idadi hii inatokana na leseni za uchimbaji ambazo ndani yake kuna wachimbaji wadogo wengi.

Hata hivyo, serikali inaanda utaratibu maalumu kwa ajili ya kuwasambazia umeme wachimbaji na itaanza kwa migodi 10 ili kuwaongezea ufanisi wa kazi zao na kuongeza kasi ya vijana kujiajiri.

Nyansiri anasema pamoja na kuwajengea uwezo na kuwa walezi wa wachimbaji, pia wanasimamia fursa za wachimbaji kupata mikopo katika mabenki kama vile matawi ya Benki ya NMB na CRDB Benki wilaya humo ambazo zimewakopesha wafanyabiashara 80 ili kukuza mitaji yao.

"Tunaishukuru Serikali. Serikali imewezesha uchimbaji wa madini ya dhababu kwa wachimbaji wa kati na wadogo hapa Chunya kwenda sawa ikiwamo kuongezeka ajira za kujiajiri, hivyo itaongeza ukuaji wa uchumi na ongezeko kubwa la kodi kwa taifa," anasema.

Aidha, anasema ofisi yake inafanya juhudi kubwa kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Mbeya, Mkuu wa Wilaya Chunya na Meneja wa Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) kuhakikisha wanatimiza malengo ya kuwasambazia umeme kwa kuanzia migodi 10 ya wachimbaji wa kati ikiwamo mgodi wa Gold Tree Tanzania Ltd na Steven Nyondo.

"Serikali itawasambazia umeme katika migodi 10 ili kuwapunguzia gharama za uendeshaji na kuwaongezea ufanisi katika uzalishaji, kipato cha mmoja mmoja kitaongezeka, uchumi pia utakua na taifa litapata faida kubwa kupitia madini ya dhahabu tofauti na sasa uzalishaji ni mdogo kutokana na kutumia mchakato mrefu," anasema.

Akifafanua zaidi anasema Chunya imepewa hadhi ya kuwa Mkoa wa Kimadini kutokana na kuzalisha madini ya dhahabu kati ya kilo 200 mpaka 250 kwa mwaka huku ikiwa na wachimbaji wa kati 70 na wadogo zaidi ya 300.

"Leseni moja ndani yake inakuwa na wachimbaji wadogo wengi, tunalazimika kupambana kuwapa mwongozo na elimu mara kwa mara ili kupunguza maafa mbalimbali yasiyokuwa na lazima, ikiwamo kuondoa wafanyabiashara wanaouza pombe," anasema na kuongeza.

"Kazi ni kubwa tunahakikisha tunapambana kutoa elimu japo kuna usiri lakini tunakabiliana nao kuepusha utoroshaji wa madini isivyo halali unaoinyima serikali mapato halali," anasema ofisa huyo.

Anasisitiza kwamba kuna vituo maalumu vya kuuza madini ya dhahabu yanayopatikana katika migodi na kwamba bado kuna changamoto ya uelewa unaogubikwa na usiri lakini wanazunguka kila kona kuwasaka na kuhakikisha wanaojaribu kutorosha madini hawafanikiwi.

"Sisi Chunya tunazingatia na kufuata maelekezo ya Rais Samia, wachimbaji wadogo asilimia 99 wamewekeza kwenye uchimbaji wa dhahabu, tunawasisitiza kupeleka dhahabu sokoni ili kodi yote inayopatikana iingie kwenye ujenzi wa taifa, mafanikio na juhudi za Rais tunayaona na Watanzania wamemuelewa jemedari wetu," anasema Nyansiri.

Meneja wa Mgodi wa Gold Tree Tanzania Ltd, George Zakaria, anaelezea hali ya upatikanaji wa dhahabu kwa sasa kuwa imeshuka ikilinganishwa na awali ambapo mgodi ulikuwa unatoa gramu kati ya 100 na 200 lakini sasa uzalishaji umeshuka na kufikia gramu 40 kwa siku.

Anasema mgodi huo una mashimo 16 yanayozalisha dhahabu kwa sasa baada ya kufukia mashimo sita ya awali kutokana na dhahabu kumalizika.

Anasema wao kama wachimbaji wa kati wanazalisha dhahabu mbichi ambayo mchakato wa kuvunja mwamba mpaka kupata jiwe ukikamilika inapimwa uzito kwa kufuata taratibu zilizowekwa na Tume na kuorodheshwa katika kitabu maalumu na baadaye inapelekwa kwenye mauzo katika soko lililowekwa na serikali.

"Sisi tunachimba dhahabu mbichi tunaipima hapa na kutoa risiti itakayompa mwenye dhahabu hiyo kuuza kwenye soko lililowekwa na serikali, tukifikisha kwenye soko kule wanaichoma kupitia mitambo maalumu ikiwa dhahabu iliyoiva," anasema meneja huyo.

Anasema serikali iwafikirie wachimbaji wadogo na kuwawezesha katika vikundi ili waongeze mitaji.

"Serikali ishuke chini kwa wachimbaji wadogo ituwezeshe mitaji kupitia vikundi tuongeze nguvu ya kujiajiri na kukuza pato la taifa," anasema Zakaria.

Siasa

# Mbunge aipigia 'saluti' Serikali ya Awamu ya Sita



**Na Lauden Mwambona, Vwawa**

JAPHET Hasunga, ni Mbunge wa Jimbo la Vwawa lililopo Wilaya ya Mbozi mkoani Songwe.

Wilaya ya Mbozi ina majimbo mawili ambayo ni Mbozi na Vwawa ambalo Hasunga ni Mbunge wake.

Hasunga, msomi wa masuala ya Uhasibu, amewahi kuwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii na pia Waziri wa Kilimo kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tano na hivi sasa yupo kipindi cha pili cha ubunge wake.

Lakini kwa mtazamo wake, anasema Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ni ya aina yake na`inaupiga mwingi' kwa jinsi inavyopeleka fedha kwenye miradi vijijini.

Anaitoa kauli hiyo mbele ya wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Jimbo lake aliouitisha hivi karibuni Mjini Vwawa ili kutoa taarifa ya kazi zilizofanywa na serikali pamoja na yeye mwenyewe kuanzia Desemba 2020 hadi Aprili, 2023.

Mkutano huo aliouitisha, ulihudhuriwa na wajumbe zaidi ya 700 wakiwemo viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya.

Hasunga anasema katika kipindi cha miaka mitano kuanzia Novemba 2020 hadi Oktoba 2025, CCM imepanga kutekeleza malengo makuu sita.

Katika kitabu chake cha taarifa chenye kurasa 58, anataja mambo hayo kwamba la kwanza ni kulinda na kuimarisha misingi ya utu, usawa, haki na uongozi bora ili kuimarisha amani, umoja na mshikamano wa taifa.

Anasema katika hili, Serikali ya Awamu ya Sita imetekeleza kwa vitendo kwa kuhakikisha vyombo vyote vya kulinda nchi na usalama vinaendeshwa na kwa kuzingatia sheria na vinapata mahitaji yao muhimu.

Mbunge huyo anataja lengo la pili la CCM kwamba ni kukuza uchumi wa kisasa, fungamanishi, jumuishi na shindani uliojengwa kwa msingi viwanda huduma za kiuchumi na miundombinu wezeshi.

Anafafanua kwamba, katika suala hili, Serikali ya Awamu ya Sita imefanya kwa juhudi kubwa kuhakikisha Watanzania wote wanashiriki kwa vitendo katika kujenga uchumi huku ikiweka mazingira mazuri ya uwekezaji kwa watu kutoka nje na wa ndani ya nchi.

Hasunga anataja lengo la tatu la CCM kwa miaka mitano hadi 2025 kwamba ni kuleta mageuzi ya kilimo, mifugo na uvuvi ili kuwa na uhakika wa chakula na kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya uchumi.

Anawaeleza wajumbe kwamba Serikali ya Awamu ya Sita katika kutekeleza hili, imetoa mbolea ya ruzuku kwa wakulima wote wakiwamo wakulima zaidi ya 40,000 wa jimbo lake.

Anasema pia imeanzisha mradi wa Jenga Kesho Bora (BBT) na kwamba hata kwenye Mifugo, serikali imeruhusu mashamba yake yawe ya mfano kwa mifugo huku sekta ya uvuvi nayo ikipewa fedha nyingi kuboresha miundombinu.

Hasunga ambaye jimbo lenye lina kata 18, anasema lengo la nne la CCM kwa miaka mitano hadi 2025, ni kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za afya, elimu, maji, umeme na makazi vijijini na mijini.

Katika lengo hili, Hasunga anawauliza wajumbe: "Ni nani ambaye hajaona mabadiliko katika sekta hizo?." Swali hilo linajibiwa na wajumbe wote wakisema "Hakuna asiyeona majengo kwani sekta zote zimejaa mabadiliko mengi kuelekea kwenye ubora.

Mbunge wa Vwawa anaendelea kutaja malengo akisema la tano ni kuchochea matumizi ya utafiti, sayansi na teknoloji na ubunifu kama nyenzo ya maendeleo ya haraka ya kijamiii na kiuchumi na kwamba lengo la sita ni kutengeneza ajira zisizopungua milioni nane katika sekta rasmi na zisizo rasmi nchini.

Hasunga anasema katika malengo haya, Serikali ya Rais Dk. Samia, imeimarisha utafiti wa mambo mengi hususan masuala ya utafiti wa mbegu bora za mazao mbalimbali nchini.

Anasema pia ameweka mazingira ambayo Watanzania wengi wanawekeza kwa kujenga vitega uchumi vingi vikiwamo vya hoteli, viwanda vidogo vidogo, taasisi binafsi huku wengine wakianzisha mashamba ya kilimo na ufugaji ambayo yameongeza ajira kwa vijana.

Mambo makubwa yametendeka katika Jimbo la Vwawa lenye watu 240,703 kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 lina shule za msingi 98 zikiwamo za watu binafsi nane na sekondari 36 ambapo za serikali ni 24.



Mbunge Hasunga anasema Serikali ya Awamu ya Sita, imeendelea kuboresha elimu na kusababisha ufaulu kuongezeka.

Pia anataja sekta ya afya kwamba jimbo lake lina zahanati 41, vituo vya afya sita, Hospitali moja ya Wilaya na Hospitali moja ya Mkoa.

Anasema Serikali ya Awamu ya Sita, imeleta fedha nyingi katika sekta ya afya zikiwamo Sh. bilioni 13 kwa ajili Hospitali ya Mkoa pekee na pia imeleta zaidi ya Sh. bilioni 14.9 nyingine kwa sekta ya afya kwa jumla.

Kuhusu masuala ya maji, anasema miradi mbalimbali ya maji kupitia Wakala wa Maji Vijijini (Ruwasa) na Mamlaka ya Maji Mbozi na Mlowo (Vwamasa) ambapo zaidi ya miradi 10 imetekelezwa ikigharimu zaidi ya Sh. bilioni tano.

Anasema ujenzi wa barabara za lami nao umeshika kasi katika jimbo hilo na kwamba mapato ya Halmashauri nayo yameongezeka.

Jimbo la Vwawa ndani ya miaka miwili na nusu hadi Aprili, mwaka huu, limepata majengo ya kisasa ya mahakama ya mkoa na wilaya mpya, limepata Kituo cha Redio kimoja Vwawa Fm na kwamba uzalisha mazao nao umeongezeka kwa kiasi kikubwa kutokana na wananchi kupata mbolea ya ruzuku.

Hasunga kupitia taarifa yake anasema karibu kila kijiji katika kata zote 18, imepokea fedha za serikali, mbunge, madiwani na wahisani kwa ajili ya kazi za maendeleo.

Anawapongeza madiwani wa kata zote, Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi na wananchi kwa michango yao ya hali na mali katika maendeleo.

Hasunga ameorodhesha orodha ya kata na vijiji vyote vilivyopokea fedha za maendeleo za serikali, wahisani, Mfuko wa Bunge na za kwake mwenyewe

Katika orodha hiyo, Mbunge ameziorodhesha kata zote ambazo zimepokea wastani wa zaidi ya Sh. bilioni moja kuwa ni Isalalo, Msia, Nyimbili, Hasanga, Ichenjezya, Vwawa, Ilolo, Hasamba, Ipunga na Kata ya Ukwile. Kata zingine ni Kilimapimbi Nanyala, Ihanda, Mlangali, Ruanda, Idiwili, Hezya na Kata ya Iyula.

## MADIWANI WAMPA MAUA YAKE RAIS SAMIA NA MBUNGE

Akizungumza kwa niaba ya madiwani wote kwenye mkutano huo, Diwani wa Kata ya Nyimbili, Tinson Nzunda, anaiomba CCM kuendelea kumuamini Rais Dk. Samia 2025 na kwamba madiwani wa Jimbo la Vwawa wote wameweka alama ya vema kwa Rais Samia na Mbunge wao Hasunga.

Naye Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Mbozi, Leopard Mlawizi, akizungumza kwa niaba ya Chama kwenye mkutano huo, anaishukuru Serikali ya Awamu ya Sita,

Mbunge Hasunga na madiwani wa kata katika jimbo hilo kwa kutekeleza vema na kuisimamia Ilani ya CCM. Mlawizi anasisitiza kwamba CCM ni Chama dume na itaendelea kuisimia vema serikali yake.

Siasa



# Katiba Mpya, tuhakikishe ni mhimili imara wa nyumba ya Watanzania - 1

**Na Dk. Felician B. Kilahama**

MUNGU wetu ni mwema sana, mwingi wa rehema na fadhili zake kwetu ni za milele hivyo, tumshukuru kwa yote na kulitukuza jina lake kwa jinsi anavyotulinda na kutukingia hatari zote za kiroho na kimwili.

Mchakato wa kupata Katiba Mpya nchini Tanzania, ulianza zaidi ya iliyopita.

Jaji mstaafu Joseph Warioba na timu husika, walifanya kazi nzuri ya kukusanya maoni kutoka kwa wadau wengi nchi nzima.

Hata hivyo, kwa sababu ambazo Watanzania walio wengi hawazifahamu, mchakato wa kutayarisha Katiba Mpya, ukasitishwa.

Hivyo, jitihada za kuipata Katiba Mpya zikapungua nguvu, lakini kumekuwepo na vuguvugu na mapendekezo kutoka kwa baadhi ya Watanzania hususani wanasiasa hasa kambi ya upinzani kwamba Katiba Mpya ni muhimu kwa maslahi mapana ya taifa letu.

Sasa kuna msukumo wa pekee kwamba Katiba Mpya iwe ni matokeo ya maridhiano na ikamilike kwa matarijio kuwa iweze kutumika wakati wa Uchaguzi Mkuu Oktoba, 2025. Nia yao ni njema kwa msingi kwamba taifa liwe na uhakika maslahi ya wengi yanalindwa na Katiba na kwa faida ya wote.

Hii ni pamoja na kuona kuwa kuna Tume huru ya kuendesha na kuusimamia uchaguzi na kutenda haki.

Kadhalika, isiingiliwe na mtu yeyote katika kutimiza majukumu yake kwa kuzingatia misingi ya Katiba pamoja na Sheria ikiwemo kanuni zitakazohususika na uendeshaji uchaguzi.

Wapo baadhi ya Watanzania ambao wangependa kuona wakati wa uchaguzi uja, 'mgombea binafsi' asiyeambatana na chama chochote cha siasa, anachangamkia haki hiyo Kikatiba.

Mimi ni raia wa kawaida kwa maana kwamba sina ujuzi wowote kuhusu masuala ya Katiba na Sheria, isipokuwa, natambua kwamba Katiba ndiyo Sheria Mama/Msingi Mkuu wa kuendesha na kuisimamia nchi kiutawala na kijamii.

Kutokana na hali hiyo, sheria nyingine zote zitakazotumika nchini hazitakiwi, kwa namna yoyote ile, kupingana/kukinzana na Katiba ya nchi.

Isitoshe, nimekuwa nikiona na kushuhudia umuhimu wa Katiba kwa taifa letu kuwa viongozi wa juu, ukianzia Rais pamoja na wasaidizi wake hasa anaowateua; huwa wanalazimika kuapa kuwa 'wataitetea' na 'kuilinda' Katiba. Pamoja na nia njema hiyo, binafsi huwa najiuliza hivi ni kweli huwa 'wanaitetea' na 'kuilinda' Katiba au Katiba ndiyo 'inayowatetea' na 'kuwalinda' wao? Hebu tutafakari kwa nianjema ya kuimarisha maslahi mapana na kwa faida ya wengi kutokana na Katiba kuwa ndiyo 'chombo' kikuu cha kuliongoza taifa letu.

Tanzania inafahamika duniani kwamba ni nchi huru na salama



yenye mipaka inayoeleweka na kuheshimiwa kitaifa na kimataifa.

Kwa msingi huo, mimi naliona eneo hilo, ndani ya mipaka sahihi isiyo na utata wowote, kuwa ni 'nyumba' muhimu sana; yenye kutoa hifadhi kamilifu kwa Watazania wote.

Ndani yake, asilimia 65 ya watu wote wanaishi vijijini na asilimia 35 wanaishi mijini na katika majiji.

Vijiji na vitongoji vyake, pamoja na miji na majiji, ni sehemu za makazi ya watu takribani milioni 61.7 (Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022).

Idadi hiyo ndiyo wananchi husika wanaoishi na kuhifadhiwa ndani ya 'Nyumba' ijulikanayo, Tanzania.

Ndani ya 'nyumba' nzima kwenye vijiji na maeneo mengine miji na majiji, kuna kaya mbalimbali zilizojenga makazi yao chini ya 'dari' la nyumba' mama inayoitwa Tanzania.

Hatahivyo, ili nyumba iwe imara na salama kwa watu waishio humo, ni lazima ijengwe kwenye msingi imara usioweza kusababisha iyumbe hata kama kutakuwepo na dhoruba kali, nyumba husika ibaki kama ilivyojengwa na kuwahakikishia usalama wanaoishi humo na mali zao.

Kwa mtazamo wangu, Katiba ya taifa letu, ndiyo "nguzo kuu/msingi wa nyumba yetu."

Hivyo, msingi huo unatakiwa uwe imara kweli kweli kama ni zege liwe lenye saruji ya kutosha, kokoto na mchanga kamilifu. Isitoshe, usimamizi wake unatakiwa, wakati wote, uwe imara na thabiti na usioyumbishwa na chochote kile kilicho chini ya jua; isipokuwa kutii na kunyenyekea kwa Mamlaka Takatifu iliyo juu mbingu, yaani Mungu Mwenyezi.

Ninachokisema namaanisha Katiba tarajiwa, ilenge kuimarisha musitakabali mzima wa taifa letu kwa misingi kwamba tuwe

na chombo kisichotiliwa shaka na yeyote na kiwe na thamani ya kutumika muda mrefu hata kama ni zaidi ya miaka 100 ijayo, kwa maslahi mapana ya taifa letu na wakazi wake.

Mwenyezi Mungu aliumba binadamu wa kwanza mwanaume hivyo Adamu akawa mzaliwa wa kwanza katika uso wa dunia. Maandiko Matakatifu yanatuambia kwamba, Mungu

alisema: "Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatawale samaki wa baharini na ndege wa angani, na wanyama na nchi yote pia, na kila kiumbe kitambaacho juu ya nchi.

"Bwana Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, akampulizia puani pumzi ya uhai; mtu akawa nafsi hai". Bwana Mungu hakuishia hapo, bali pia alienda zaidi akaweka bustani upande wa Mashariki mwa Edeni.

Bustani hiyo ilisheheni miti ya aina mbalimbali iliyotamanika kwa macho na kufaa kwa kuliwa" (matunda yake).

Vilevile, akaweka "mti wa uzima katikati ya bustani na mti wa ujuzi wa mema na mabaya.

Bwana Mungu akamtwaa huyo mtu, akamuweka katika bustani ya Edeni, ailime na kuitunza.

Bwana Mungu akamuagiza huyo mtu akisema "matunda ya kila mti waweza kula, lakini matunda ya mtu wa ujuzi wa mema na mabaya, usile (agizo), kwa maana siku utakapokula

matunda ya mti huo, utakufa hakika."

Hata hivyo, Bwana Mungu akasema: "Si vyema huyo

mtu awe peke yake, nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye.

Ndipo Bwana Mungu akamfanyia kutoka katika ardhi kila aina ya wanyama wa msituni, na kila ndege wa angani akamletea Adamu ili aone atawaitaje; kila kiumbe hai, jina

alilokiita Adamu, likawa ndilo jina lake.

Adamu akawapa majina yao kila mnyama wa kufugwa,

na ndege wa angani na kila mnyama wa mwituni. Pamoja na hayo yote, hakuonekana wa kufanana naye maana walikuwa ni wanyama na ndege tu.

Kwa msingi huu, Adamu ndiye binadamu wa kwanza: Akawa ni 'lango' kwa binadamu wengine. Kuletewa wanyama na ndege ili awape majina ilikuwa ni ishara muhimu katika 'kumiliki na kutawala'.

Kutokana na kutokuwepo aliyefanana naye, ndipo Bwana Mungu akaikumbuka ahadi yake kwamba alikwishasema kuwa 'si vyema mtu huyu awe peke yake, nitamfanyia wa kufanana


naye' (ni kweli wanyama na ndege, hakuna unayeweza kumlinganisha na binadamu aliyeumbwa kwa mfano na sura yake Mungu).

Ndipo Bwana Mungu akamletea Adamu 'usingizi mzito',

naye akalala; kisha akatwaa ubavu wake mmoja, akafunika nyama mahali pake, na 'ule ubavu alioutwaa katika Adamu Bwana Mungu akaufanya mwanamke akamleta kwa Adamu'. Naye Adamu alipomuona yule mwanamke akasema: "Sasa huyu ni mfupa katika mifupa yangu, na nyama katika nyama yangu, basi ataitwa 'mwanamke' kwa maana ametwaliwa katika

mwanaume."

Hili siyo jambo dogo wala la kubezwa maana ni msingi wa kiu-umbaji na unaendana na mustakabali mzima katika



Afya

# Yajue mazoezi ya kuimarisha ubongo

**Na Godfrey Sanga kwa msaada wa mtandao**

UBONGO ndiyo chombo kikuu zaidi mwilini. Kwani hudhibiti utendaji kazi kadhaa katika mwili, hutafsiri hisia zinazoingia na kudhibiti hisia kwa jumla. Pia ni kitovu cha kumbukumbu, akili na mawazo.

Kadhalika, hutajwa kufanya mazoezi mengi kwa siku kuliko kiungo chochote cha mwili na shughuli fulani zinaweza kusaidia kuboresha utendaji wa ubongo na muunganisho.

Hii inaweza kusaidia kulinda ubongo kutokana na kupita kwa umri. Ubongo unafanya kazi kila wakati, hata wakati wa kulala.

Hata hivyo, shughuli fulani zinaweza kuhusisha ubongo kwa njia mpya ambazo zinaweza kusababisha uboreshaji wa kumbukumbu, utendakazi wa utambuzi, au ubunifu.

Hutajwa kuhusika katika kila kitu tunachofanya na kama sehemu nyingine yoyote ya mwili, unahitaji pia kutunzwa. Kufanya mazoezi ya ubongo ili kuboresha kumbukumbu, umakini na utendakazi wa kila siku.

**MAZOEZI YA UBONGO**

Utafiti unanyesha kuwa kuna njia nyingi unaweza kuboresha na kuongeza uwezo wa akili na kusaidia ubongo wako kuwa na afya, bila kujali umri.

Kufanya mazoezi fulani ya ubongo ili kusaidia kuboresha kumbukumbu, umakini na kuufanya ubongo wako kuwa na uwezo kadiri unavyozeeka.

**MAZOEZI YA UBONGO YENYE MATOKEO RAHISI NI KAMA IFUATAVYO:-**

**I. KUTAFAKARI**

Kutafakari kwa ujumla huhusisha kuelekeza fikra kwa njia ya utulivu na iliyodhibitiwa. Kutafakari kunaweza kuwa na faida nyingi kwa ubongo na mwili. Kulingana na utafiti, kutafakari kunaweza kunufaisha ubongo kwa kupunguza kasi ya kuzeeka kwa ubongo na kuongeza uwezo wa ubongo kuchakata habari.

**II. TASWIRA ZAIDI**

Kutafakari kwa ujumla huhusisha kuelekeza fikra kwa njia ya utulivu na iliyodhibitiwa, kutafakari kunaweza kuwa na faida nyingi kwa ubongo na mwili. Kulingana na utafiti, kutafakari kunaweza kunufaisha ubongo kwa kupunguza kasi ya kuzeeka kwa ubongo na kuongeza uwezo wa ubongo kuchakata habari.

**III. CHEZA MICHEZO YA KADI YA KUMBUKUMBU**

Kucheza michezo ya kadi au michezo ya bodi, inaweza kuwa njia ya kufurahisha ya kushirikiana au kupitisha wakati. Shughuli hizi pia zinaweza kuwa na manufaa kwa ubongo.

Utafiti mmoja uligundua uhusiano kati ya michezo na hatari ndogo ya kupungua kwa utambuzi kwa watu wazima.

Michezo ya kadi ya hujaribu kuvuta kumbukumbu ya muda mfupi ya mtu na uwezo wa kukumbuka. Ni njia rahisi na ya kufurahisha ya kushirikisha ubongo na kuwezesha maeneo yanayohusiana na utambuzi wa muundo na kumbukumbu.

**IV. FANYA MAZOEZI YA MANENO NA MAFUMBO**

Mafumbo ya maneno ni shughuli maarufu inayoweza kuchangamsha ubongo. Utafiti wa awali unabainisha kuwa mafumbo ya maneno yanaweza kuchelewesha kuanza kwa uharibifu wa kumbukumbu kwa watu walio na shida ya akili kabla ya kliniki.

Kukamilisha fumbo kunaweza kuwa njia nzuri ya kupitisha wakati, na kunaweza pia kufaidi ubongo wako. Utafiti mmoja uligundua kuwa mafumbo huwasha kazi nyingi za utambuzi, ikiwa ni pamoja na utambuzi, mzunguko wa kiakili, kumbukumbu ya kazi, hoja. Utafiti huo ulihitimisha kuwa kufanya mafumbo mara kwa mara na katika maisha yote kunaweza kulinda dhidi ya athari za kuzeeka kwa ubongo.

**V. CHEZA SUDOKU, CHESS NA CHECKERS**

Mafumbo ya nambari, kama sudoku, yanaweza kuwa njia ya kufurahisha ya kuupa changamoto ubongo. Watu wazima wenye umri wa miaka 50 hadi 93, waligundua kuwa wale waliofanya mazoezi ya mafumbo ya nambari mara nyingi zaidi walikuwa na utendaji bora wa utambuzi.

**Inaendelea Uk. 15**



# Afya

Inatoka Uk.14

## VI. KUCHANGAMANA/ KUINGILIANA

Kufurahia au kuwa pamoja na marafiki, kunaweza kuwa shughuli ya burudani inayohusisha kiakili na inaweza kusaidia kuhifadhi utendaji wa utambuzi.

Baadhi ya shughuli za kijamii zinazoweza kusaidia kuchochea ubongo ni pamoja na:

1. Kuwa na majadiliano
2. Kucheza michezo
3. Kushiriki katika michezo ya kijamii

## VII. KUJIFUNZA UJUZI MPYA

Kujifunza ujuzi mpya, hushirikisha ubongo kwa njia tofauti na kunaweza kusaidia kuboresha utendaji kazi wa ubongo.

Watu wazima waligundua kuwa kujifunza ustadi mpya na unaohitaji utambuzi, kama vile kuteleza au kupiga picha, kuliboresha utendakazi wa kumbukumbu.

## VIII. ONGEZA MSAMIATI WA KIBINAFSI

Kuongeza anuwai ya msamiati wako ni njia nzuri ya kupanua maarifa yako wakati wa kufanya mazoezi ya ubongo wako. Njia rahisi ya kujenga msamiati ni kusoma kitabu au kutazama kipindi cha televisheni na kuandika maneno usiyoyafahamu. Kisha mtu anaweza kutumia kamusi kutafuta maana ya neno hilo na kufikiria njia za kutumia neno hilo katika sentensi.

## IX. JIFUNZE LUGHA MPYA

## X. SIKILIZA MUZIKI

Kusikiliza muziki ambao mtu anafurahia, hushirikisha na kuunganisha sehemu mbalimbali za ubongo. Watafiti wanapendekeza kwamba hii inaweza kusababisha uboreshaji wa kazi ya utambuzi na ustawi wa jumla.

## XI. JIFUNZE KUCHEZA ALA YA MUZIKI

Kujifunza ala huchochea sehemu za ubongo zinazowajibika kwa kazi ya pamoja. Kucheza ala kunaweza kunufaisha ukuaji wa utambuzi katika ubongo mchanga na kusaidia kulinda dhidi ya kupungua kwa utambuzi katika ubongo unaozeeka.

## XII. FANYA HOBBIES ZA KUVUTIA

Kuchukua hobby mpya kunaweza kuchangamsha kiakili na kufanya mazoezi ya ubongo wako kwa njia mpya.

## XIII. ZOEZI MARA KWA MARA

Mazoezi ya kimwili ya mara kwa mara yanasaidia ubongo na mwili. Mazoezi huboresha vipengele vifuatavyo vya kumbukumbu ya afya ya ubongo, utambuzi, na uratibu wa magari.

## XIV. DANCING

Kulingana na Vituo vya Kudhibiti na kuzuia Magonjwa (CDC), mazoezi yana athari za manufaa kwa vipengele vifuatavyo vya kumbukumbu ya afya ya utambuzi, mipango, na shirika. Ngoma ni aina ya mazoezi ambayo inaweza pia kuhusisha maeneo ya ubongo yanayohusika katika mdundo na usawa.



## XIV. KUCHEZA MICHEZO

Michezo fulani inadai kimwili na kiakili. Baadhi zinahitaji ujuzi mbalimbali wa utambuzi, kama vile uangalifu endelevu, kupanga na kufanya kazi nyingi. Wanariadha wasomi wanaoshiriki katika michezo inayohitaji sana huwa na umakini bora na kasi ya usindikaji wa habari haraka.

## XV. FANYA MAZOEZI YA TAI CHI

Tai chi ni aina ya mazoezi ya mwili ambayo yanajumuisha harakati za mwili laini, kupumua kwa mdundo na kutafakari. kazi ya ubongo na muunganisho kati ya watendaji wa tai chi na wale ambao hawakufanya mazoezi.

Watafiti waligundua kuwa watendaji wa tai chi walikuwa wameboresha muunganisho kati ya maeneo tofauti ya akili zao. Walipendekeza kuwa hii inaweza kuboresha utambuzi na kupunguza kiwango cha upotezaji wa kumbukumbu.

## XVI. KULALA

Ingawa si lazima mazoezi ya vitendo, usingizi ni muhimu kwa ubongo na mwili. Kulingana na Taasisi ya Kitaifa ya Matatizo ya Neurological and Stroke, watu wazima wengi wanahitaji kulala kwa saa saba na tisa kila usiku, ingawa watu wengi hupata usingizi mchache kuliko wanavyohitaji.

Usingizi umeonyeshwa kuongeza kumbukumbu ya kumbukumbu, kupunguza uchovu wa kiakili na kudhibiti kimetaboliki. Kwa hiyo, kuhakikisha unapata usingizi wa kutosha kila usiku ni hatua muhimu katika kudumisha ubongo wenye afya.

## MAZOEZI YA MAFUNZO YA UBONGO KWA WATOTO NA VIJANA

Unapowatazama watoto na watu kwa jumla, ni rahisi kuona kwamba sote tuna tofauti katika jinsi akili zetu zinavyounganishwa na kufanya kazi.

Hapa kuna baadhi ya shughuli unazoweza kufanya na mtoto wako ili kukuza ukuaji wa ubongo wenye afya ambayo itaboresha utendaji kazi kadhaa muhimu. Kwa njia, mazoezi haya yatasaidia sio tu kwa watoto, lakini pia kwa watu wazima.

Kufanya mazoezi ya kupumua kwa kina (lifti ya kupumua au kuhamisha pumzi kwenye maeneo yote ya mwili) husaidia kuboresha kumbukumbu na udhibiti wa akili.

Inaelezwa kuwa watoto wanapenda kufanya hivi, fanya mara nyingi. Anza kwa kumfanya mtoto wako kuketi katika nafasi ya kuvuka-mguu au amelala na kupumua kawaida.

## NJIA NANE UNAZOWEZA KUBORESHA AFYA YA UBONGO.

- Zoezi
- Unywaji kahawa
- Mwanga wa jua
- Kujenga miunganisho yenye nguvu
- Kutafakari
- Kulala vizuri
- Kula vizuri
- Kucheza tetris

## VYAKULA VINAVYOFAA KWA UBONGO

Uchambuzi unaonyesha kuwa chakula sahihi cha ubongo ndicho kinacholinda moyo na mishipa ya damu, ikiwa ni pamoja na yafuatayo:

- Kijani, mboga za majani
- Samaki yenye mafuta
- Berries
- Chai na kahawa
- Walnuts

## VYAKULA SABA VIBAYA ZAIDI KWA UBONGO.

- Vinywaji vya sukari
- Wanga iliyosafishwa
- Vyakula vyenye mafuta ya trans
- Vyakula vilivyosindikwa sana
- Pombe
- Samaki ya juu katika Mercury

## JE, MAZIWA YANAFAA KWA UBONGO?

Uwiano kati ya ulaji wa maziwa na viwango vya kioksidishaji asilia kinachoitwa glutathione kwenye ubongo, umepatikana kwa watu wazima wenye umri mkubwa na wenye afya.

## JE, TUFAHA LINAFAA KWA UBONGO?

Tufaha ni kamili kwa kuweka mwili na akili salama! Matokeo kadhaa ya utafiti yamehusisha kula tufaha na utendakazi bora wa ubongo, ikiwa ni pamoja na kupungua kwa mwanzo wa matatizo ya mfumo wa neva kama vile Alzheimers na Parkinson.

## ULAJI WA KUKU NI MZURI KIAFYA?

Kuku ni chanzo kamili cha protini, hutoa usawa wa ubongo, na ni chanzo cha chakula cha choline na vitamini B6 na B12.



Afya

# Ngozi hueleza uhalisia wa afya ya ndani ya binadamu



**Hatua ya kwanza ya kulinda ngozi ni kujikinga na jua. Kuvaa shati, kupaka mafuta, kuvaa kofia (kapelo), miwani ya jua na kupata mahali penye kivuli.**

UTAFITI wa hivi karibuni unaonesha kuwa ngozi ya binadamu inaeleza mambo mengi kuhusu mitindo ya maisha.

Huonesha athari ya kuvuta sigara, kunywa pombe, kuchomwa na jua na kuishi maisha ya dhiki.

Utafiti wa Baltimore Longitudinal. ulifuata maelfu ya wanaume (watu wazima (na baadaye wanawake), kwa miongo kadhaa, ili kuona jinsi afya zao zilivyobadilika na jinsi zilivyoathiriwa na jeni na mazingira yao.

Miongo miwili tu baadaye, wanasayansi walikuwa tayari wamefanya uvumbuzi wa kuvutia wanaume wasio na utulivu wa kihisia wana uwezekano mkubwa wa kupata ugonjwa wa moyo.

Matokeo ya kushangaza zaidi yalithibitisha kile ambacho kimeshukiwa kwa muda mrefu; jinsi unavyoonekana ni kipimo sahihi cha afya yako ya ndani.

Kufikia 1982, wanaume ambao mwanzoni mwa utafiti, walionekana kuwa wakubwa kwa umri wao walikuwa na uwezekano mkubwa wa kufa miaka 20 baadaye.

Hii inaungwa mkono na utafiti wa hivi karibuni zaidi, ambao uligundua kuwa wagonjwa ambao wanaonekana wamezeeka miaka 10 kuliko wanavyopaswa, asilimia 99 wana na matatizo ya afya.

Afya ya ngozi inaweza kutumika kutabiri idadi ya kadhaa ya matatizo ya kiafya.

**UMRI NA NGOZI.**

Kuna njia kuu mbili za kupima umri wa mtu. Ya kwanza ni ile ya kawaida. Lakini pia kuna umri wa kibiolojia, ambayo inaonyesha kiwango cha kuzeeka kimwili (ukomavu wa viungo na seli).

Lakini ni mazingira husababisha uharibifu ngozi. Mionzi ya ultraviolet B (UVB), inaweza kuharibu DNA - kusababisha saratani ya ngozi.

Asilimia 95 ya mionzi ya ultraviolet inayofika kwenye uso wa dunia, ni ultraviolet A (UVA).

Miale ya jua inaweza kupenya ndani kabisa ya ngozi. Ultraviolet unahusishwa na zaidi ya asilimia 80 ya mabadiliko yanayoonekana kwenye ngozi.

Mwaka 2000, dhana mpya iliibuka, kikundi cha wanasayansi kutoka Chuo Kikuu cha Bologna, Italia, kilipendekeza njia mpya ya kufikiria kuhusu kuzeeka.

Kinga za mwili kwa vijana,



huzalishwa ili kudumisha utaratibu.

Lakini kadiri twanavyozeeka, uzalishwaji huu huja na kemikali zenye nguvu katika mwili na kuharibu seli zenye afya.

Vilevile kemikali tunazotumia, hupunguza unene wa ngozi, kuzalisha makunyanzi na kupunguza unyumbufu wa ngozi.

Kwa upande mwingine. kemikali inayotolewa na ngozi ikiwa haina kazi, huingia kwenye damu, ambapo huenea na kuharibu tishu nyingine.

Kemikali kutoka kwenye ngozi zinaweza kufikia na kuharibu viungo vinavyoonekana kuwa havihusiani, kutia ndani moyo na ubongo.

Matokeo yake ni kuzeeka kwa kasi na hatari kubwa ya kupatwa na magonjwa.

Ngozi iliyozeeka au yenye ugonjwa, imehusishwa na magonjwa ya moyo na mishipa, kisukari cha aina ya 2 na kupungua uono pamoja na magonjwa mengine.

Ingawa inafahamika hatari za kuvuta sigara, kunywa pombe, kula kupita kiasi na kutofanya mazoezi, pia huchangia afya mbaya ya ngozi.

**KULINDA NGOZI**

Hatua ya kwanza ya kulinda ngozi ni kujikinga na jua. Kuvaa shati, kupaka mafuta, kuvaa kofia (kapelo), miwani ya jua na kupata mahali penye kivuli.

Kulinda ngozi kutokana na jua ni bora sana katika kuzuia dalili zinazoonekana za kuzeeka.

Pia, kujilinda kunazuia maambukizi mengi ya mionzi wakati wa kuzeeka na magonjwa ya uzeeni.

Lakini hii si njia pekee za kuweka ngozi katika hali nzuri.

Njia rahisi zaidi ya kuboresha afya ya ngozi ni kupaka mafuta. Na kuna ushahidi wa moja kwa moja kwamba hii inapunguza magonjwa ya ngozi.

Mbali na kuwa na mikunjo isiyosawazika, ngozi iliyozeeka na jua, huwa kavu zaidi. Viwango vya unyevu kwenye ngozi hufika kilele katika umri wa miaka 40.

Wakati ngozi imekauka, kazi zake za kuzuia maambukizi na sumu za mazingira, huwa ngumu zaidi.

Viungo vingi vya asili vinaweza kusaidia.

Kunywa maji zaidi kunaweza kusaidia kuweka ngozi kuwa na unyevu zaidi.

Kwa hiyo, kuilinda ngozi kuna faida yake, lakini ni muhimu kuipa unyevu pia.



Na Paul Mng'ong'o

KLINIKI YA FIKRA

mngongopaul@yahoo.com

# Mambo makubwa matano ya kuzingatia kwenye maisha

KAMA ukiyapa nafasi ya pekee na kipaumbele mambo haya matano tunayoyataja hapa, maisha yako yatakuwa ya baraka na amani.

1. Fanya maamuzi ya dhati kuzingatia afya yako.
2. Fanya bidii ya dhati kukuza uchumi wako.
3. Jenga maarifa na ujuzi kila siku.
4. Hakikisha unakuwa na hekima.
5. Mpende na mtegemee Mungu.

**1. KUHUSU-AFYA**

Afya ndiyo mtaji wa maisha yako. Bila afya, mambo yako muda si mrefu yatasimama kutokana na matatizo ya kiafya. Mambo ya msingi kuhusu afya ni:-

A. Ulaji sahihi – Ni vizuri kula vyakula vyenye virutubisho sahihi na kuepuka sumu mbalimbali. Vitu vikubwa vya kuepuka kwenye ulaji ni:-

- Matumizi makubwa ya wanga mwilini
- Matumizi makubwa ya mafuta. (Yanayoganda na Yasiyoganda)
- Matumizi makubwa ya sukari.
- Matumizi ya dawa yasiyo na ushauri wa wataalam.
- Zingatia unywaji wa maji ya kutosha

B. Mtazamo sahihi – Mtazamo sahihi ni mtazamo chanya. Ni vizuri ujifunze kufikiri kwa mtazamo chanya na achana na fikra zinazokuletea maumivu.

C. Kufanya mazoezi - Mazoezi ni jambo muhimu la kuimarisha afya.

D. Kupumzika - Unapaswa kupata muda mzuri na wa kutosha wa kupumzika.

**2. KUHUSU MAFANIKIO KIUCHUMI**

Mafanikio ya kiuchumi ni zao la uamuzi madhubuti wa kuishi kwa kufuata misingi na kanuni sahihi za kiuchumi. Hakuna njia ya mkato zaidi ya hii. Kuna misingi na kanuni kubwa nne za mafanikio kwenye maisha: -

A. Uamuzi thabiti – Njia za mafanikio ni ngumu na mara nyingi zinavunja moyo na kukatisha tamaa.

Njia hizi zinahitaji kujikana na kuachana na mambo mengine, hivyo si kitu rahisi.

B. Mpango thabiti

Ili kufanikiwa, lazima uwe mtu wa kupanga mambo yako na kuyasimamia sawasawa na mpango. Panga kila kitu, mfano: -

- Panga vizuri jambo/ mambo ya kufanya
- Tambua makusudi ya msingi ya jambo husika
- Panga rasilimali zako na mgawanyiko wake
- Tambua na upange mahitaji ili kufanikisha
- Panga wahusika wa jambo kwa sifa na uwezo wao
- Weka vipaumbele
- Panga matumizi sahihi ya muda
- Panga muda unaokusudiwa
- Gawanya muda kwenye vipindi vya tathmini
- Panga viashiria vya matokeo kusudiwa
- Tambua maeneo ya uwezekano wa kushindwa na uyapangie mbinu za suluhu n.k.

C. Jitihada

Mafanikio bila kufanya kazi kwa juhudi, ni sawa na kuyaimba tu mafanikio na kamwe mafanikio halisi hayatatokea.

D. Mtandao itakayokusaidia

Ili kufanikiwa kiuchumi lazima uwe na mtandao (uzungukwe) na watu sahihi watakaokusaidia kukua.

E. Bahati/Fursa

Pamoja na yote, njia ya mafanikio inahitaji bahati kwa lugha ya kijamii au fursa kwa lugha ya kiuchumi. Hapa tunazungumzia mambo makubwa matatu: -

- Upate fursa,
- Uzione fursa, na
- Uzitumie fursa kwa usahihi.

**3. KUHUSU MAARIFA NA UJUZI**

Maarifa na ujuzi ni maelezo ya kinadharia na ya vitendo, ukweli au ujuzi ambao tunapata kupitia uzoefu au kwa kujifunza. Maarifa yetu yanaongezeka tunapopata uzoefu zaidi. Ujuzi uliokuzwa vizuri unaweza kutufanya kuwa wataalam katika uwanja fulani. Ujuzi unaweza kujifunza pia.

**4. KUHUSU HEKIMA**

Hekima ni zao la matumizi ya mjumuiko wa elimu sahihi, ufahamu mzuri, ujuzi, maarifa na uzoefu kwenye kutazama na kutathmini mambo.

Mtu anayefikiria kwanza kabla ya kusema au kutenda na akatenda sawasawa, huyo anahesabika mwenye hekima.

Kuna watu wengi wanapata hali hii kwa kutokana na vyanzo mbalimbali kama vile: -

- Mazingira aliyokulia
- Watu wanaomzunguka
- Miongozo au Misingi anayoiamini
- Kutembea maeneo mengi
- Mambo mengi aliyoona au kukutana nayo
- Elimu na uelewa

Hekima ndiyo ulinzi wa mafanikio tunayokuwa tumeyajenga. Matatizo mengi kwenye maisha ni matokeo ya kufanya maamuzi bila ya kutumia hekima.

**5. KUHUSU MUNGU**

Siri kubwa ya watu waliofanikiwa na wengi kuwa imara (thabiti) kwenye maeneo yao (siri ambayo haitajwi sana), ni kumtegemea na kumcha Mungu wao.

Maisha bila Mungu, ni maisha ya utupu yasiyo na mwelekeo.

**HITIMISHO:**

Hakuna uhaba wa maarifa kwenye zama tunazoishi sasa, maarifa yapo tele na yanapatikana kwa urahisi kabisa.

Unaweza kujua chochote unachotaka kujua.

Kinachokosekana ni juhudi kupata maarifa sahihi na kufanyia kazi yale maarifa ambayo mtu unapata.


Kama ungependa kupata ushauri au usimamizi wa karibu katika kuishi mwongozo huu, (unaweza kuwa taasisi binafsi au ya serikali, kikundi cha kijamii, kanisa, umoja, NGO, mtu binafsi n.k.) basi karibu sana, nitashirikiana nawe kwa neema na msaada wa Mungu.

*Karibu tuwasiliane kwa namba 0676055444 au barua pepe mngongopaul@yahoo.com na kwenye mitandao ya kijamii.*

Paul Mng'ong'o
*Your Partner in Growth.*



**MWENYEZI MUNGU TUNAKUOMBA DUA UMPE MAISHA MAREFU, AFYA NJEMA, NGUVU ZAIDI NA MAFANIKIO, RAIS WETU MPENDWA DK, SAMIA SULUHU HASSAN**



# ECCAS yaisimamisha uanachama Gabon




**LIBREVILLE, Gabon**

JUMUIYA ya Uchumi ya Afrika ya Kati (ECCAS), imeamua kusimamisha unachama wa Gabon kufuatia mapinduzi ya kijeshi ya Agosti 30, mwaka huu yaliyomuondoa madarakani Rais Ali Bongo.

ECCAS inatoa taarifa hiyo baada ya kikao chake kilichofanyika juzi katika Mji Mkuu wa nchi jirani ya Guinea ya Ikweta, Malabo.

Rais wa Guinea ya Ikweta, Teodoro Obiand Nguema, alisema Gabon ni kitisho kwa amani, usalama na uthabiti katika nchi nyingine wanachama wa ECCAS.

Hatua hii inafuatia jana kuapishwa kuwa Rais Jenerali Brice Oligui Nguema, aliyeongoza mapinduzi ya Gabon kama wa mpito, akiahidi uchaguzi huru, wazi na wa kuaminika kwa lengo la kurejesha utawala wa kiraia, lakini hakutaja tarehe maalumu.

DW



## Rais Kim atarajia kukutana na Putin

**NEWYORK, Marekani**

MAREKAANI imesema Kiongozi wa Korea Kaskazini, Kim Jong Un, anatarajia kukutana na Rais wa Urusi, Vladimir Putin, kuzungumzia kuhusu kuipelekea silaha Urusi kwa ajili ya vita vyake nchini Ukraine.

Tangazo hilo lilitolewa baada ya Ikulu ya Marekani, kutahadharisha wiki iliyopita kwamba Urusi kwa njia ya siri, ilikuwa tayari ikifanya mazungumzo na Korea Kaskazini kupata silaha kadhaa na mahitaji mengine kwa juhudi zake za vita.

Kwa mujibu wa vyombo vya habari nchini Marekani, Kim huenda akasafiri mwezi huu kwenda Vladivostok mji wa wa pwani ya bahari ya Pasifiki ambao hauko mbali na Urusi, kukutana na Rais Putin.

Vyombo hivyo, vimeripoti kuwa Kim pia huenda akasafiri kwenda mjini Moscow, lakini hilo halina uhakika.

Urusi na Korea Kaskazini, hazijasema lolote kuthibitisha mkutano kati ya viongozi wao.

DW.

## Nyusi hawezi kushtakiwa UK'



**MAPUTO, Msumbiji**

RAIS wa Msumbiji, Filipe Nyusi, hawezi kushtakiwa nchini Uingereza kwa madai ya kukubali malipo kinyume cha sheria.

Malipo hayo ni kuhusiana na kesi ya nchi hiyo dhidi ya benki ya Credit Suisse na wengine kuhusu kashfa inayojulikana kama `tuna bond' ya Dola bilioni mbili, Mahakama Kuu ya London, iliamua juzi.

Kesi ya sakata ya Tuna Bond, ambayo pia imepewa jina la `deni lililofichwa,' imefanya uchunguzi wa jinai kutoka Maputo hadi New York pamoja na msururu wa kesi zinazouwiana mjini London zinazohusisha taasisi ya Credit Suisse, Kampuni ya ujenzi wa meli ya Privinvest, mmiliki wake Iskandar Safa na wengine wengi.

Privinvest na Safa walijaribu kumuingiza Rais Nyusi kwenye kesi hiyo, wakisema kwamba anapaswa kuchangia fidia yoyote ambayo wanaweza kuagizwa kulipa ikiwa watapatikana na hatia nchini Msumbiji, lakini Mahakama Kuu iliamua juzi kwamba Rais Nyusi ana haki ya kupata kinga ya serikali.

## Rais wa Iran asifu mataifa ya Afrika

**OUAGADOUGOU, Burkina Faso**

RAIS wa Iran, Ebrahim Raisi, juzi alizipongeza nchi za Afrika kwa kupinga ukoloni.

Kwa mujibu wa vyombo vya habari, Rais Raisi alitoa pongezi hizo wakati wa mkutano na Waziri wa Mambo ya Nje wa Burkna Faso, Olivia Rouamba, mjini Tehran, akiyasifu mataifa ya Afrika kwa kupinga ukoloni ingawa hakuitaja Ufaransa moja kwa moja.

Burkina Faso na Mali zilikuwa koloni za Ufaransa zinaongozwa na makundi ya kijeshi ambayo yalivunja uhusiano wao na taifa hilo, na kisha kuimarisha uhusiano wao na Russia.

Nchini Niger ambako kundi la kijeshi lilifanya mapinduzi Julai, mwaka huu, bado kuna maandamano ya kuvitaka vikosi vya Ufaransa nchini humo viondoke.

Kupitia taarifa iliyondikwa kwenye tovuti rasmi ya Rais wa Iran, Raisi alisifu kile alichokitaja kuwa mwamko mpya.

Wakati wa kikao na Rouamba, Raisi alielezea azma ya Iran kushirikiana na mataifa rafiki ya Kiafrika.

Rouamba kwa upende wake, alisema kwamba Burkina Faso iko tayari kuimarisha ushirikiano wake na Iran.

Katika miaka ya karibuni, Iran imekuwa ikiimarisha uhusiano na Bara la Afrika kama juhudi ya kupunguza kutengwa, pamoja na kupunguza makali ya vikwazo ilivyowekewa tangu 2018 baada ya Marekani kujiondoa kwenye mkataba wa nyuklia.

Julai mwaka huu, Raisi alizitembelea Kenya, Uganda na Zimbabwe.

VOA.



## 40,000 wahudhuria kuapishwa Mnangagwa




**HARARE, Zimbabwe**

RAIS wa Zimbabwe, Emmerson Mnangagwa, aliapishwa juzi baada ya kutetea kiti chake kwa kuhudumu kwa muhula wa pili baada ya uchaguzi uliozua utata, ambapo aliibuka mshindi dhidi ya mpinzani wake mkuu, Nelson Chamisa.

Watu 40,000 walimshangilia Mnangagwa alipowasili kweye Uwanja wa Taifa wa michezo mjini Harare.

Akihutubia umati uliohudhuria, aliwashukuru wananchi wa Zimbabwe kwa kuwa na uchaguzi wa amani na uwazi na aliahidi kutumia rasilimali za asili za nchi yake ili kuongeza uzalishaji na kuugeuza uchumi wa nchi.

Mnangagwa anaonekana kuwa ana kibarua kizito mbele yake, wakati taifa lake likikabiliwa na mfumuko mkubwa wa bei duniani na kuwa na sarafu ambayo inakaribia kutokuwa na thamani kabisa.

Katika sherehe hizo, Mnangagwa alipigiwa mizinga 21 na kikosi cha wanajeshi wa Zimbabwe, kuashiria mwanzo wa muhula wake mpya.

Kiongozi huyo aliingia madarakani kwa mara ya kwanza mwaka 2017 baada ya kumuondoa kiongozi wa muda mrefu Robert Mugabe na kisha baadaye akashinda kwenye uchaguzi uliozua utata mwaka uliofuata.

Katika uchaguzi wa mwezi uliopita, mwanasiasa huyo mwenye umri wa miaka 80, alimshinda mpinzani wake mkuu, Nelson Chamisa (45), kutoka chama cha Citizens Coalition for Change (CCC), kulingana na matokeo ambayo sasa yanapingwa na upinzani.

Kiongozi wa chama cha CCC, Tendal Biti, alisema anaona hatari mbele iwapo matokeo ya uchaguzi huo hayatabatilishwa.

VOA.

# Tunafuga 'majini' Uwanja wa Taifa ili yale nyama



Na Petter Mwendapole

MOJA ya sababu kubwa za kupewa nafasi kwa mashindano ya CAF Super League kufanyika kwenye ardhi yetu ni jinsi mashabiki wa soka wa Tanzania wanavyopenda mpira wa miguu.

Hili limejionyesha mara kadhaa wakati klabu zetu hususani za Simba na Yanga zinaposhiriki mashindano ya kimataifa, ndipo ule mzuka wa timu hizo unapopanda zaidi.

Shirikisho la Soka Afrika (CAF) hata lile la dunia (FIFA) limekuwa likiangalia fan Base (ukubwa/kiwango cha mashabiki) wa nchi fulani katika kuipatia majukumu ya kimataifa.

Lakini ukubwa huu wa mashabiki ambao umekuwa ukiongezeka kila iitwapo leo na kuweka msisimko mkubwa kwenye ligi na mashindano mengine kama ambavyo zamani ilikuwa kwenye mashindano ya Taifa Cup ambapo timu za mikoa zilikuwa zikichuana kuwania ubingwa, ushindani ulikuwa mkali sana.

Watu wengi walikuwa na uzalendo na timu zao na hii ilipelekea kupata timu ya taifa imara ambayo ilikuwa na mkusanyiko wa vipaji kutoka mikoa yote. Hii haikujalisha kuangalia wachezaji kutoka timu za ligi kuu pekee, maana mikoani walikuwa wana ligi zao ambazo zilikuwa zinachuana na kutoa wachezaji wa hatari.

Naikumbuka timu ya mkoa wa Kagera ikiitwa Rwelu Eagles ambayo ilikuwa moto katika miaka ile ya themanini na ikijizolea mashabiki, kwa wale waliokuwa wakisikiliza mpira huo Redioni ililkuwa raha zaidi mtangazaji wa zamu awe Charles Hillary Nkwanga.

Kilichokuwa kikitokea uwanjani na kusimuliwa kwenye radio kilifanya mashabiki kesho yake kugombea magazeti ili kupata taarifa za undani juu ya nini kilitokea uwanjani.

Idadi ya watu ambao walikuwa waliokuwa wakihudhuria uwanjani ilikuwa kubwa si Dar es Salaam bali hata mikoa mingine, japo inaonekana kwa sasa idadi imekuwa kubwa zaidi kutokana na promo ambazo zimekuwa zikifanyika.

Wakati wa mechi ya Yanga iliyofanyika kwenye Uwanja wa Taifa tulishuhudia mashabiki wakivunja geti ili kuingia uwanjani, tukashuhudia shabiki mmoja akifariki na wengine kujeruhiwa.

Hawa walikuwa wanalazimisha kuingia Uwanjani kwa nguvu kutokana na kutokuwa na tiketi na hata waliokuwa nazo walilazimika kukaa kwenye foleni muda mrefu.

Katika Tamasha la Simba Day tuliambiwa tiketi zimeisha baada ya kuwa zimenunuliwa zote. Baadae tukaambiwa watu 2000 walizuiwa kuingia uwanjani.

Pamoja na hao 2000 bado kulikuwa na malalamiko mengi zaidi ya hao waliotajwa kuzuiwa wakidai wana tiketi na wanaambiwa Uwanja umejaa hivyo hawawezi kuingia.

Tulioangalia tamasha kupitia televisheni tuliona watu wakiwa wamekaa watatu watatu katika siti mbili kwa maana alikuwa mtu mmoja anaongezeka katikati.

Uzoefu wa mechi za Simba na Yanga ndio balaa zaidi, mashabiki wanalipa tiketi tena za VIP na bado wanakaa kwenye ngazi kwa maana ya kuwa nafasi za kukaa hakuna.

Changamoto hii si mara ya kwanza kutokea, lakini inaonekana wahusika pengine hawajapata muarobani wa tatizo au wanafanya kusudi kwa kuwa nao wana maslahi yao.

Zama za kuishi maisha ya makomandoo, jamaa walikuwa wanakuwa na pesa nyingi zaidi baada ya mechi kuliko hata wachezaji, na pale uwanja wa Taifa kulikuwa na baa maarufu kwa Chichi, wao ndio walikuwa wanaongoza kwa kununulia watu pombe.

Miaka imeenda Makomandoo hawana nguvu tena na mfumo wao umeondoka taratibu ingawa bado changamoto ya tiketi imeendelea kubaki, changamoto ya uwanja kujaa na watu kukosa sehemu ya kukaa bado imeendelea kubaki.

Hivi tunashindwaje kutengeneza mfumi wa kununua tiketi kwa mtandao, kwa mfano kadi kama za Selcom. Kadi ina jina namba ya simu, na unaponunua tiketi itaonyesha muda wa tiketi iliponunuliwa na siti ambayo shabiki huyu anakwenda kukaa.

Mfumo kama huu unatumika siku hizi kwenye mabasi ya mikoani, unanunua tiketi na unachagua siti yako, kwanini Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Bodi ya Ligi, Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo na Baraza la Sanaa wasiangalie changamoto.

Tuliona taasisi hizi zikifanya kazi kwa pamoja wakati tatizo la umeme lilipotokea kwenye mechi kadhaa za CAF na kusababisha mpaka watu kupoteza kazi zao.'

Hivi ni kweli hatuwezi kufanya lolote hadi maafa yatokee ndio tuchukue hatua? Leo tunafurahia CAF wametupa nafasi ya Super League, kesho tutalalamika tutakapozuiwa kuruhusu mashabiki Uwanjani.

Tutakuwa wepesi wa kulalamika na kutafuta mchawi wakati haya 'majini' tunayafuga wenyewe ili yale damu na nyama baadae. Siku zote tumesema kinga ni bora kuliko tiba.

Kununua chandarua cha sh 10,000 ni rahisi zaidi, kuliko kulipia kitandani hospitali, kwenda kumuona mgonjwa hospitalini mara tatu kwa siku na kuhakikisha unapika chakula amacho huna hata uwezo nacho.

Wanasema Mchelea Mwana kulia, hulia mwenyewe.





# Choki asepa na Kijiji




MWANAMUZIKI Ally Choki 'Mzee wa Farasi' amesepa na kijiji katika onyesho lake la kwanza tangu ajiondoe katika bendi ya Twanga Pepeta aliyoitumikia kwa takribani miaka miwili.

Ilikuwa ni katika ufunguzi wa ukumbi wa New Mawasiliano Park ambapo mwanamuziki huyo alialikwa kutumbuiza na bendi wenyeji Tukuyu Sound chini yake Kalala Junior.

Choki na Kalala wamewahi kuimba pamoja bendi ya Mchinga Generation 'G8', African Stars na baadae Twanga Pepeta.

Katika onyesho hilo ambalo muda mwingi Choki alikuwa akiimba na mashabiki waliokuwa wamefurika, aling'ara zaidi na nyimbo zake za Jirani na Aminata ambazo alitunga akiwa Twanga. Lakini baada apanda jukwaani na Komandoo Hamza Kalala na kukumbushia enzi za bendi ya Bantu Group ambapo walipiga wimbo Vicky.

Mwanamuziki huyo alisisitiza kwa sasa yuko huru na hana mkataba na bendi yoyote hivyo mwaliko wowote wa kazi hana kizuizi.



## Papii kuikamata Makumbusho?

BAADA ya kutoonekana jukwaani kwa takribani mwezi mmoja, Papii Kocha 'Mtoto wa Mfalme' Ijumaa anatambulishwa rasmi katika ukumbi wa Kijiji cha Makumbusho, Dar es Salaam.

Mwanamuziki huyo anatambulishwa rasmi jukwaani na bendi ya Town Classic Band akiwa kama Rais wake huku akitambulisha pia nyimbo nne mpya ndani ya bendi hiyo.

Sambamba na Papii aliyekuwa mmoja wa wamiliki wa bendi ya Tukuyu Sound, Town Classic pia itawatambulisha wapiga magitaa wawilii elombee Kichinja na Babaa Bass.

Wanamuziki hao wameondoka na Papii kutoka Tukuyu ambao kwa maelezo msanii huyo hao ni wapiga ala wake.

Macho na masikio yatakuwa Makumbusho kuona staili atakayoingia nayo Papii aina ya shoo itakayofanyika na uwezo wa kumiliki jukwaa na kujaza watu.

## Beta Musica kama inakuja vile...







"AII mamamaaa Chaliee, chalii naomba chenji mamaa, chenji ya mia chalii, chenji ya dola chalii, shilingi, ngumu kwa kupata na mambo ya DAR ni sokotosokoto."

MOJA ya bendi ambayo ilitingisha nchi kwa muda mfupi ni Beta Musica 'Wana Telema'.

Za chini chini zinasema kuna ujio mpya wa bendi hiyo ambayo pamoja na nyimbo lukuki ilizokuwa nazo lakini kibao chake ambacho kimeendelea kuishi mpaka leo ni Bana Beta.

Taae=rifa zinasema vikao vya awali vimeanza kufanyika juu ya ujio wa bendi hiyo iliyoanzishwa baada ya wanamuziki kumeguka kutoka Dar Musica ambao awali waliwa wanamuziki wa Diamond Sound.

Mbali na Bana Beta, bendi hiyo ilikuwa na nyimbo zingine kama One Day Yes, Bomengo, Panadol, Manzese Kariakoo, Kalundakala, Angela, Sumbungengi, iliundwa na wanamuziki kama Ibonga Katumbi, Richard Mangustino, King Blaise, Mule Ziri, Totoo Ze Bingwa, Papii Kocha.

Wengine ni Kardinali Gento, Elly Chinyama, Dizinne Bakunde. Seif Controller, Marcis Mengi, George Kuba, Marie Nyembasi, Salima Abeid, Zawadi Mwambimbi, Elizee, Mila Yesa Mbombo, Nguza Mbangu.

Beta walishiriki kampeni za uchaguzi wa CCM mwaka 2000 mwanzo mwisho wakimpigania mgombea Urais wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Amani Abeid Karume.

Kwa sasa baadhi ya wanamuziki waliokuwa wakiunda bendi hiyo wameacha muziki wa dansi na kuwa watumishi kwenye makanisa ndani na nje ya nchi huku wawili Donaa Zinganguvu na Zawadi wakiwa wamefariki.

# Ruto apokea Kombe la Ubingwa la EPL




**NAIROBI, Kenya**

RAIS William Ruto wa Kenya amepokea ujumbe kutoka Chama cha Soka cha England ambao ulimtembelea Ikulu, mjini Nairobi.

Kiongozi huyo ambaye ni shabiki mkubwa wa soka, alikutana na ujumbe huo uliokuwa umebeba Kombe la Ligi Kuu ya England maarufu kama EPL ambao ulikuwa ukifanya prmosheni ya michuano hiyo.

Hata hivyo haijaelezwa kilichungumza zaidi katika mkutano na ujumbe huo lakini inafahamika inawekana Rais alitumia nafasi hiyo kuona namna ambavyo Kenya ingeweza kutangza utalii kupitia EPL.

Ujumbe huo ulitarajiwa kuelekea nchini Rwanda ambako pia utakutana na Rais Paul Kagame ambaye ni shabiki mkubwa wa timu ya Arsenal.

Rwanda imekuwa ikitangaza nchi yake kupitia ligi hiyo katika kampeni yao iitwayo, Visit Rwanda ambapo wiki moja iliyopita imeingia mkataba mwingine na klabu ya PSG kwa ajili ya kampeni kama hiyo,

# Brazil yamtema nyota wa Man United



**SAO PAULO, Brazil**

TIMU ya Taifa ya Brazil imemtema kikosini winga wa Manchester United Antony kufuatia madai unyanyasaji yaliyotolewa na mpenzi wake wa zamani .

Shirikisho la Soka la Brazil lilisema mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 ameondolewa kwenye kikosi baada ya "mambo yake kujulikana ambayo yanahitaji kuchunguzwa.

Antony anashutumiwa kwa kumshambulia mpenzi wake wa zamani Gabriela Cavallin kwa kumpiga kwa kichwa kwenye chumba cha hoteli mjini Manchester Januari 15, na kumwacha akiwa amekchanika sehemu ya kichwa ambacho kilihitaji matibabu kutoka kwa daktari.

Shiriika la Habaru la UOL la Brazili ambalo ndilo liliandika madai yaliyotolewa na na Gabriela na Polisi mjini Sao Paulo na Greater Manchester wanachunguza madai hayo, ambayo ywameyakanushwa na mchezaji huyo.

"Ninaweza kusema kwa utulivu kwamba shutuma hizo ni za uongo na kwamba ushahidi uliotolewa tayari na ushahidi mwingine utakaotolewa unaonyesha kwamba sina hatia kwa tuhuma hizo

"Nina imani kuwa uchunguzi unaoendelea wa polisi utadhihirisha ukweli kuhusu kutokuwa na hatia," Alisema Antony

# Inter Miami yaamua kuwekeza kisawasawa



**MIAMI, Marekani**

KLABU ya Inter Miami FC ya hapa imeanza ujenzi wa uwanja wake mkubwa wa kisasa wa soka kwa ajili ya matumizi ya timu yao ambayo inashiriki Ligi Kuu ya Marekani.

Inter Miami ambayo inamilikiwa na nyota wa zamani wa Manchester United na timu ya Taifa ya England, David Beckham, imeupa jina Uwanja huo kuwa Miami Freedom Park.

Kwa mujibu wa taarifa ya timu hiyo, Miami Freedoma Park utakamilika na kufunguliwa mapema mwaka 2025.

Miami imeendelea kuwa gumzo kwa sasa sehemu mbalimbali duniani baada ya kumchukua nyota Lionel Messi ambaye awali alitarajiwa kujiunga na klabu za Saudi Arabia.

Messi amekuwa akiwekewa ulinzi wa mabaunsa uwanjani ili asibuguziwe na mashabiki ambao wamekuwa wakiruka kutaka kuingia uwanjani kumgusa.

Katika mechi ya juzi dhidi ya LAFC shabiki mmoja aliruka uzio na kuingia uwanjani ili kumgusa mchezaji huyo hali iliyofanya mlinzi wake apambane naye kumtoa.

Miami imekuwa ikitengeneza faida kubwa tangu kujiunga kwa mchezaji huyo mwenye ushawishi na wapenzi wengi duniani,




# Nyota wa Mamelodi azua mjadala

**CAPETOWN, Afrika Kusini**

MSHAMBULIAJI wa timu ya wanawake ya Mamelod Sundown, Miche Minnies amezua mjadala mitandaoni kutokana na muonekano wake.

Minnies (21) amekuwa gumzo kutokana na kufanana kwa kiasi kikuwa na nyota wa zamani wa timu ya Taifa ya Brazil, Ronaldinho Gaucho.

Hakuna taarifa zaidi juu ya uhusiano wa wawili hao lakini kwa nafasi anayocheza dada huyo muonekano wake, wengi wamekuwa wakisema huenda kuna undugu kati yao.

# CR7 aweka historia




**LONDON, England**

MSHAMBULIAJI nyota wa soka duniani, Christiano Ronaldo ameandika historia mpya ulimwenguni.

Ronaldo ameandika historia ya kupachika mabao 850 mpaka sasa katika maisha yake ya soka, idadi ambayo haijafikiwa na mchezaji mwingine yoyote.

Nyota huyo wa Ureno kwa sasa anacheza Ligi ya Saudi Arabia akiichezea timu ya Al Nassr ambayo ni moja ya klabu tajiri katika nchi hiyo.

# 'CAF Super League ni Fursa

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema michuano ya CAF Super League inayoandaliwa na Shirikisho la Soka la Afrika (CAF) na kufanyika nchini ni fursa kwa watanzania kutengeneza fedha.

Akizungumza mjini Dar es Salaam, Katibu Mkuu wa Baraza la Michezo la Taifa, Neema Msita amesema CAF wameipa Tanzania nafasi hiyo kutokana na mtaji wa mashabiki ambao iko nao.

"Hii ni fursa kwetu, timu hizi za kigeni zitakuwa kwetu na kutumia vitu vyetu kuanzia hoteli mpaka magari, wapo watu watakaopata ajira za muda mfupi, ni vizuri kila mhusika kwenye eneo lake akafanya vyema ili kuvutia nafasi kama hii wakati mwingine," alisema.

Katika michuano hiyo mikubwa barani Afrika ikijumuisha timu nane bora, Tanzania imewakilishwa na Simba huku kukiwa pia ni timu za Enyimba ya Nigeria,, TP Mazembe ya Congo, Al Ahly ya Misri, Wydad Casablanca ya Morocco.

Zingine ni Mamelodi Sundown ya Afrika Kusini, Esperance ya Tunisia na Petro du Luanda ya Angola. Kila timu imepewa zaidi ya sh bilioni 1.5 kwa ajili ya maandalizi ya mashindano hayo.

# Viongozi, Mashabiki Yanga wote kutumia basi moja




**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI wa klabu ya Yanga utasafiri na mashabiki wao kwa njia ya basi kuelekea Kigali, nchini Rwanda kwa ajili ya mechi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Barani Afrika dhidi ya El Marreikh ya Sudani.

Wakati viongozi na mashabiki wakisafiri kwa njia ya barabara, wachezaji wa timu hiyo wataondoka kwa ndege kuelekea mjini Kigali ambapo pambano litafanyika kwenye Uwanja mpya wa Pele.

Meneja Uhusiano wa Yanga, Ally Kamwe alisema gharama za kwenda na kurudi nchini Rwanda zitakuwa sh 150,000 ambazo hazijumuishi chakula wala malazi.

Alisema msafara wa kwenda huko utaondoka Septemba 14 ambapo mechi itakuwa Septemba 16. Mashabiki hao wanatarajiwa kuwasili Rwanda Septemba 15.

Wakati Yanga wakiweka wazi gharama za kwenda Kigali, klabu ya Simba wao wamelazimika kuongeza basi la pili kwa ajili ya kwenda Ndola, Zambia kwa mashabiki wanaotaka kushuhudia mechi kati ya timu hiyo na Power Dynamos ya huko.

Gharama ya kwenda na kurudi Ndola ni sh 200,000 ambapo basi la kwanza lilishajaa nab ado maombi yameendelea kuwa mengi juu watu wanaotaka kwenda huko.

# Geita yatenga Bilioni 1 zaidi za Uwanja wao



Inatoka Uk.24

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Zahara Michuzi alisema uwanja huo umekwishakamilika kwa asilimia 80.

"Katika kuhakikisha tunatekeleza maagizo ya Rais kwa vitendo, Geita tumekwishaanza kujenga uwanja na uko katika hatua nzuri, katika kuuboresha tumeongeza sh bilioni moja ambayo itatumika kumalizia sehemu iliyobaki," alisema.

Zahra alisema Uwanja huo utakuwa na sehemu ya mazoezi kwa maana ya GYM, utakuwa na vyumba vya wachezaji kulala maarufu hosteli lakini huduma zingine ambazo zinatakiwa kwa timu kuwa nazo.

"Geita itakuwa moja ya timu ambayo ina viwanja bora kabisa vya michezo nchini, Rais alitoa agizo la kujenga viwanja na sisi tumetekeleza kwa vitebndo ifikapo mwakani tunaamini uwanja utakuwa umekamilika na kuanza kutumika," alisema.

Kwa sasa timu ya Azam ndio ina uwanja wake wa kisasa ambapo pamoja na kutumiwa na klabu hiyo, lakini imekuwa ikiukodisha pia kwa vikosi vingine ili kutumia.

Azam inachaji sh milioni tano kwa kila mchezo ambao timu nyingine inataka kutumia uwanja huo lakini pia ina chaji kiwango kingine endapo timu inataka kuweka kambi ya mazoezi hapo.

# Wavu watakata Afrika

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya Taifa ya mpira wa wavu kwa wanaume, Almasi King imekung'uta Mali seti 3-1 katika michuano ya Mataifa ya Afrika, inyaoendelea nchini Misri.

Ushindi wa jana umefufua matumaini ya watanzania hao, kusonga mbele ambapo leo inahitaji kushinda mechi dhidi ya wababe Tunisia.

Seti ya kwanza ilishuhudiwa Almasi wakiibuka na ushindi wa pointi 25-18, seti ya pili 25-22 wakati seti ya tatu, Mali wakageuka kibao kushinda pointi 25-17.

Almasi walikaa vyema katika seti ya nne kwa kuibuka na ponti 26-24 na kuzuia mechi hiyo kwenda seti ya tano.

Katika mechi ya kwanza iliyofanyika juzi, Almasi ambao walitoa upinzani katika seti ya pili na ya tatu. Walipoteza pambano hilo kwa kipigo cha seti 3-0.

Katika seti ya kwanza, Chad walishinda pointi 23-19 huku seti ya pili Almasi waliweza kuwabana wapinzani wao na kufungwa pointi 33-31. Seti ya mwisho Almasi waliendelea kutoa upinzania lakini bahati haikuwa yao kwani walipoteza tena kwa pointi 25-23.

Mechi ya leo djidi ya Tunisia itanza saa nane mchana kwa saa za Afrika Mashariki.



# Quattara wa Simba aenda UAE

**Na Mwandishi Wetu**

Mlinzi wa zamani wa Simba SC, Mohamed Ouattara amejiunga na klabu ya Al-Ain FC inayoshiriki Ligi Kuu ya Falme za Kiarabu (UAE) kwa mkataba wa mwaka mmoja.

Ouattara (24) raia wa Ivory Coast alisajiliwa na aliyekuwa kocha wa Simba Zoran Maki msimu uliopita kabla ya kuachana na timu hiyo msimu huu.

Mchezaji huyo alikuwa mmoja wa wanasoka ambao walielezwa kiwango chao kilikuwa kidogo na usajili wao uliigharimu Simba kutokana na kuwalipa mishahahara na mahitaji mengine bila kuitumikia klabu.




# Ihefu wampa Thank You Simkoko




**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA John Simkoko ameondolewa kuinoa timu ya soka ya Ihefu ya Mbalali mkoani Mbeya.

Hakuna maelezo zaidi yaliyotolewa juu ya kuondolewa kwa kocha huyo ambaye aliisaidia timu hiyo katika msimu uliopita wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

elekeo
poti
Leo yetu ndiyo kesho yetu
|Jumatano Septemba 6 - 12, 2023|


## Quattara wa Simba aenda Uarabuni



## Brazil yamtema nyota wa Man U

Uk. 22





# Presha ya Robertinho yashuka

**Na Mwandishi Wetu**

ILE presha aliyokuwa nayo Kocha wa timu ya soka ya Simba, Robertinho Oliveira dhidi ya kile kilichopewa jina UKUTA wa Berlin sasa imeshuka rasmi.

Hatua hii inatokana na mlinzi tegemeo na kipenzi cha kocha huyo, Henock Inonga kupona jeraha la mkono na kuanza majukumu yake ikiwa ni pamoja na kuitwa kwenye kikosi cha timu ya Taifa ya Congo.

Inonga amekuwa nje tangu mechi ya kwanza ya ngao ya hisani ambapo aliumia mkono Simba ikipambana na Singida Fountain Gate. Mechi hiyo iliisha kwa mikwaju ya penalti ambazo Simba ilisonga mbele.

Simba ilianza kuona pengo la nyota huyo katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara, baada ya kupachikwa mabao mawili ya haraka haraka na Mtibwa katika ushindi ambao Simba walipata mabao manne.

Kocha Robertinho aliweka wazi kuwa hakuna beki bora kwake katika Afrika Mashariki na Kati kama Inonga na kwamba endapo angekuwepo kwenye mechi hiyo basi ukuta wao usingetikisika.

Lakini jana nyota huyo ambaye aliwahi kuifunga Yanga, aliripoti kwenye kambi ya timu ya Taifa ya Congo tayari kuwakabili Sudani hapo Septemba 9.

Nyota mwingine ambaye amewahi kuichezea Yanga, Fiston Mayele ajiunga na kambi hiyo akitokea Pyramid ya Misri.



## Ihefu wampa Thank You Kocha Simkoko



Uk. 23

## Viongozi, Mashabiki Yanga kutumia basi moja

## Geita yatenga Bilioni 1 zaidi za Uwanja

**Na Mwandishi Wetu, Geita**

HALMASHAURI ya mji wa Geita imetenga sh bilioni moja kwa ajili ya kumalizia Uwanja wa timu ya soka ya Geita Gold ambao unatarajiwa kukamilika hapo mwakani.

Inaendelea Uk. 23

